

# MSIOGOPE

 Ni vizuri kurudi katika kusanyiko la Bwana, usiku wa leo, kwenye usiku huu wa Jumamosi wakati uovu mwingi sana unaendelea, daima, Jumamosi usiku ni usiku ambao Shetani hushika hatamu. Lakini kuona watu wangali wanampenda Bwana vya kutosha kujitokeza, kumtumikia, hilo ni la ajabu, hakika ninathamini hilo, ninathamini wema wenu.

<sup>2</sup> Na sasa, kesho asubuhi, sasa, ninyi wageni wote hapa, pale...shikeni njia mwende kwenye baadhi ya makanisa haya mazuri, wako hapa kwa ajili ya, wakiuwakilisha mkutano huu. Na kama unazuru hapa, mbona, chukua tu kanisa lako ulilojichagulia, kuna madhehebu mengi mbalimbali, ba—basi chukua tu mahali pako kwenye shule ya Jumapili, watafurahi sana kuwa nawe.

<sup>3</sup> Na halafu kesho alasiri, nafikiri saa nane tunaanza ibada. Nami nafikiri waliutangazia kwanza saa tisa, nao wanajua mimi ni mhubiri mwenye maneno mengi sana, kwa hiyo nafikiri walishikwa na hofu na kuupanga ili kwamba twende kanisani kesho usiku. Kwa hiyo, njoni saa nane kesho alasiri, na ndipo tutajaribu kuachilia wakati ufaao ili mweze kwenda nyumbani mkale ninii yenu...Ni nini huku juu? Ni *chakula cha jioni* huku juu au *chakula cha kutwa*? Huh? Mimi—mimi huchanganya hilo kabisa. Mnaona, kwangu mimi kingekuwa ni *chakula cha jioni*. Kama—kama—kama ningekula chakula changu cha kutwa wakati huo, basi nitapata chakula changu cha jioni saa ngapi? Mnaona? Ni—ni—ninakosa mlo mahali fulani, na—nakipenda tu, *chakula cha jioni*.

<sup>4</sup> Wanasema, “Umekosea, Ndugu Branham.” Loo, la, hilo ni la Kimaandiko, kamwe hamli *chakula cha kutwa* cha Bwana, mnakula *chakula cha jioni* cha Bwana. Hiyo ni kweli. Hakukuwako na—na chakula cha kutwa, hakikutajwa, kilikuwa ni chakula cha jioni cha Bwana. Njia hizi za kujifanya walizo nazo siku hizi haziambatani na Biblia, mnaona, katika njia zetu za kale za Kentucky kule chini, tunakotoka. Loo, tuna chakula cha kutwa, kiamshakinywa, na chakula cha jioni. Na kwa hiyo, kesho alasiri... .

<sup>5</sup> Jambo fulani lilienda mrama mahali fulani basi, vema, kama nimekosea, mimi ninaninii tu, nililelewa tu vibaya, mnaona, nadhani. Kwa hiyo ilikuwa ni chakula cha kutwa, kiamshakinywa, na chakula cha jioni nyumbani kwetu, Baba aliingia...Kiamshakinywa, chakula cha kutwa, na chakula cha jioni, hiyo ni kweli, nilijua kulikuwa na kasoro mahali fulani, nikasema jambo fulani. Mke wangu, alisema, “Unaweza kusema

mambo mengi sana vibaya.” Na hiyo ni kweli, hakika amesema kweli hapo.

<sup>6</sup> Baadhi ya matangazo: Kama kanisa lenu halina ibada, wakati fulani juma lijalo, tutakuwa papa hapa Ohio, huko, pamoja na Ndugu Sullivan na hao wengine, ambako tumekuwa mara nyingi sana. Nafikiri ni kwenye Ukumbi wa Manispaa kule, nasi tungefurahi sana kuwa pamoja nanyi.

<sup>7</sup> Sasa, hebu tuone, jina la mji huo ni Middletown. Ninataka kuuita Milltown, hapo ndipo Bwana alipofanya mwujiza mkuu wakati mmoja nilipokuwa mchungaji wa kanisa la Kibaptisti, huko Milltown. Lakini ni Middletown, nililiandika *Milltown*, lakini Middletown, Ohio, nasi tungefurahi kuwa nanyi kule. Halafu basi, lakini kama kanisa lako lina ibada, sasa, wewe dumu kwenye wajibu wako.

<sup>8</sup> Ninaamini ninamjua mhubiri aliyeketi hapa, huyo ni Ndugu Hall, sivyo, kutoka huko chini Tennessee? Ilitokea tu kwamba nimekuona hapo, Ndugu Hall. Bwana akubariki. Nina furaha kukuona hapo.

<sup>9</sup> Nami nafikiri aliyeketi hapo kando ni mmoja wa wale ndugu, waliokuwa kwenye mahojiano ya faragha asubuhi ya leo. Hiyo ni kweli? Hapo, wa pili hapo, huyo . . . ? Nilifikiri, nilimtambua.

<sup>10</sup> Mnaona, tuna mahojiano ya faraghani. Huenda mkashangaa jinsi wanavyokuja, lakini kuna yapata mia sita kwenye orodha ya wanaongojea sasa. Sio tu kutoka mji mmoja. Kama kuna mji mmoja tu . . . Hii ni ulimwenguni kote, watu wanakuja kutoka kote ulimwenguni, nao wanajiandikisha miezi na miezi na miezi kabla ya wakati wa kuja huku. Watu ambao inawabidi kujua ili kuendelea, kile Neno la Mungu lilicho kwao. Nasi tunakutana nao, na kukaa tu papo hapo pamoja nao mpaka Bwana atakaponena na kusema yale wanayopaswa kufanya.

<sup>11</sup> Sasa, mnasema, “Hilo—hilo ni . . .” Mbona, bila shaka hilo ni la Kimaandiko, hiyo ni kweli kabisa. Na, bila shaka, tunatambua hiyo ni ofisi ya kinabii, ambapo sidai kuwa nabii yeyote wa Bwana, lakini hata hivyo, Yeye ameniruhusu kujua mambo, na kuniambia mambo ya kuwaambia watoto Wake kuwasaidia; hajawahi kunipungukia bado.

<sup>12</sup> Kwa mfano, mtu huyu aliyeketi papa *hapa* asubuhi ya leo . . . Sasa walifika mahali hapo . . . Na wengine wako hapa, pia, wao, baadhi yao huandika na kupata mialiko hii ili kwamba tunapokuwa karibu na mji, vema basi, wanaleta mialiko hii, naye katibu wa hudumani hana budi kuwatambua hao, kwa sababu tumewaahidi, nasi tunawaingiza mchana, na hiyo ndiyo sababu ninakuja kwa ajili ya ibada usiku, tayari nimepata maono mengi sana, karibu inakuua.

<sup>13</sup> Nawe unaweza kumwuliza yeyote wao aliye kwenye mikutano iliyo kwenye hayo mahojiano ya faraghani, jinsi Roho Mtakatifu anavyokuja na kuanika mambo, ambayo hakuna

ajuaye ila Mungu pekee. Mambo, anawaambia watu hayo, huko nyuma walipokuwa watoto wadogo, na hiyo ni—hiyo ni tofauti na ilivyo hapa jukwaani.

<sup>14</sup> Hapa jukwaani, ni ninii tu, unaona tu jambo fulani, na kulina, na kuendelea, kwa sababu huna budi kumwendea mwingine. Lakini kwa njia hii unapopata labda wawili au watatu kwa siku, siku nzima, basi unakaa tu hapo mpaka Roho Mtakatifu atakapofunua jambo hilo lote. Si lazima waseme neno moja, Yeye huwaambia, Mwenyewe, yale wamefanya, wana shida ya namna gani, wanayopaswa kufanya, na kuwasimulia maisha yao, kuwaambia yale ambayo yametendeka, na kadhalika.

<sup>15</sup> Ni wangapi wamewahi kuwa katika mahojiano hayo, wanaojua hiyo ni kweli? Inueni mikono yenu, ambao wamekuwa, naam, mnaona, kuna wengi wao hapa. Basi jamaa *huyu* ameinua mkono wake, na wengineo, tangu tumekuwa hapa.

<sup>16</sup> Anarudi moja kwa moja utotoni na kulianika papo hapo, anakwambia mahali ulipokosea na ni nini. Kama wewe ni mwaminifu mbele za Bwana, Naye ananipa hilo, sasa, hivyo ndivyo tu ninavyoweza kufanya hilo, simwongozi, ananiongoza, mnaona, i—inahitaji wewe kuliadini.

<sup>17</sup> Lakini kuna mara nyingi ambapo watu hupata shida sana, tunajua jambo la kwanza, kama Neno la Mungu litalitua, dumu papo hapo pamoja na Neno la Mungu, maana hilo ni Neno la Mungu. Lakini sasa, vipi kama umefanya kosa maishani, ama umefanya jambo fulani, ama hujui la kufanya, na halafu, hujui mapenzi ya Bwana ni nini? Unaona? Basi una haki ya kuja na kumwomba Yeye.

<sup>18</sup> Mnakumbuka wakati mmoja katika Biblia kulikuwako, naamini ilikuwa ni mwana wa Yese, aliyekuwa amepoteza, Yese alikuwa amepoteza nyumbu fulani, walikuwa wamepotea? Wao wakasema, “Tungeshuka kwenda kwa mwonaji kama tungekuwa na zawadi ya kumpa,” nao walikuwa waaminifu katika hilo, “naye angetwambia mahali pa kwenda tuwapate.” Na ndipo tunaona, ya kwamba yule mwonaji alikutana nao mtaani na kuwaambia nyumbu walikuwa tayari wamerudi nyumbani. Ndipo akaenda kumtia Daudi mafuta awe mfalme. Na sehemu nyingi sana katika Biblia, ambapo walienda mbele za watumishi wa Bwana kutaka shauri.

<sup>19</sup> Vema, sasa, ninataka kuwaulizeni: Vipi kuhusu ninyi, mnapovurugika kabisa katika matatizo, hivi hamumwendei mchungaji wenu? Hiyo ni kweli? Mnapaswa kufanya hivyo. Ukipata shida, unapaswa kumwendea ndugu yako na kumwambia, useme, “Ndugu, ni—nilikosea, si—sikupaswa kufanya hivyo. Na—nawaomba mnisaidie sasa kuomba kabisa mpaka ni—nimalize kitu hiki.” Ama, “Mnisaidie katika matatizo yangu.” Hiyo si ndiyo njia ya Kimaandiko ya kulifanya? Vema, hiyo ni kwa sababu yeye ndiye mchungaji wenu, yeye ndiye

anayewaongoza, yeye ndiye awapaye Chakula mpate ku—kula. Naye anajua jinsi ya kuwalisha kondoo wake, ambao Mungu na Roho Mtakatifu amemfanya mwangalizi juu ya hilo kundi, kuwalinda na kuwatunza, na hiyo ndiyo kazi yake.

<sup>20</sup> Vema, jambo lile lile. . . Mnaona, mimi si mhubiri, mnajua hilo. Mimi tu, sina elimu ya kutosha kuwa mhubiri. Lakini Bwana, ninapenda kuwaambia watu yale ninayojua kumhusu Yeye. Halafu basi, lakini karama yangu katika Mungu ni kitu kingine.

<sup>21</sup> Ninaangalia papa hapa ameketi hapa mbele yangu, mwingine, aliyekuwa mkutanoni asubuhi ya leo, mojawapo ya hiyo mikutano, ndugu Mbaptisti, mke wake Mmethodisti. Ndugu huyu Mbaptisti alikuwa na wakati mgumu sana wa kuacha sigara. Kwa hiyo, aliendelea kushuka kuja, na kuendelea mbele, na akaendelea kukaza mwendo. Na—na ni mtu mzuri, sisemi hivyo kwa sababu ameketi hapa, imetokea tu nimemwona yeye na mke wake.

<sup>22</sup> Na kwa hiyo, hatimaye siku moja, alipokuwa huko chini, Jeffersonville, akingojea moja ya hayo mahojiano ya faraghani, Roho Mtakatifu aliingia moja kwa moja na kufunua hilo jambo lote, na kuzihukumu sigara ambazo alikuwa amejaribu, alikuwa ameomba, alikuwa ameziweka chini. Tangu wakati huo hukugusa hata moja. Hiyo ni kweli, Ndugu Artez? Ama, jina lako ni nani? [Ndugu Arnette anasema, “Arnette.”—Mh.] Arnette. Anatoka ninii, huku chini kusini, mahali fulani ndani. [“Columbia, Carolina ya Kusini.”] Columbia, Carolina ya Kusini. Na imekwisha tangu wakati huo, sivyo? Naam, ni, hiyo ni kweli.

<sup>23</sup> Na sasa, asubuhi ya leo alikuwa amengoja ndipo akafanyiwa mahojiano mengine juu ya jambo fulani ambalo hakujua la kufanya. (Angalieni tu mwone kile Bwana alichosema.) Kabla hajaja mkewe alikuwa ameota ndoto, ya kile. . . alikuwa ameota ndoto, na kabla hata hawajaja, ama kusema lolote, niliwaambia hao ndugu kile atakachoniambia kuhusu ndoto hiyo, ilichokuwa tafsiri yake, kabla hawajafika huko (Hiyo si ni kweli?), kabla halijatukia, kile hasa kingetukia, na kile ndoto hiyo ilichomaanisha.

<sup>24</sup> Sisi. . . Hapa wakati fulani uliopita nilikuwa mkutanoni, nami nilikuwa. . . Ninaamini katika utakatifu wa mtindo wa kale, nami ninaamini katika—katika kutaja kile kile hasa Biblia isemacho, kukisema, hivyo tu. Haidhuru kama kinaumiza, kinaumiza, hakifanyi. . . Kama ukifanya hivyo kikatili, basi ninapaswa kwenda madhabahuni na kujiweka sawa, lakini ninalifanya kwa upendo.

<sup>25</sup> Kama ungemwona mtoto wako akifanya jambo ambalo lingemwua, si ungemsaidia mtoto huyo? Kama ingekubidi kumpa kichemsha makalio kidogo, wajua, naam, mcharaze tu sawasawa, a—a—afadhali ufanye hivyo, kuliko kumwacha huyo

mtoto auawe. Hivi hamwoni hivyo? Mbona, bila shaka, kama kweli ingekubidi kumsahihisha na kumcharaza na kumfanya ashike adabu. Vema, hivyo ndivyo Mungu anavyotufanya, na huu *Hapa* Mjeledi Wake, ni Injili, Ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, linakata kweli. Na kama mtumishi ameitwa na Mungu, hatapatana kwa Neno moja.

<sup>26</sup> Mhudumu fulani alikutana nami si muda mrefu uliopita, mtu mashuhuri sana, Daktari wa Uungu, akasema, “Ndugu Branham, mikutano yako inapaswa kugusa vituo vikuu mashuhuri.” Kasema, “Ungeweza kufikia mahali kama Jiji la New York, na—na kwa hiyo, mahali pakubwa mno.” Kisha kasema, “Tuna ndege zetu wenyewe na,” kanisa hili la kimadhehebu, kisha kusema, “tutakusafirisha kwa ndege kote ulimwenguni, kufikia tu mahali pa juu na vituo mashuhuri.” Kasema, “Huduma hiyo inapaswa kujulikana na kila mtu.” Kisha akasema, “Kuna jambo moja tu ninalotaka kukuomba ufanye,” kasema, “ juu ya mambo kadhaa tu unayohubiri, kama ungeyasahau tu hayo na kuyaweka kando.”

<sup>27</sup> Nami nikamwangalia, nikamwita kwa jina, ninaogopa kulitaja, maana wengi wenu mnamjua, nami nikasema, “Daktari, ninashangaa kwamba mtu wa kiwango chako, mtumishi wa Kristo, angemwomba mtumishi mwingine wa Kristo kupatana juu ya Neno la Mungu.” Kweli. Nikasema, “Ninashangaa unaposema hivyo.”

Akasema, “Vema, tunafikiri kwamba umekosea katika dhana yako.”

<sup>28</sup> Nikasema, “Basi nisahihisheni kwa Maandiko.” Hiyo ndiyo njia ya kufanya. Nikasema, “Basi nisahihisheni.” Mnaona? Kisha nikasema, “Nisingepatana juu ya Neno la Mungu, la, bwana.” Nikasema, “Mi—mimi . . .” Ndipo nikasema, “Na isitoshe . . .”

Akasema, “Vema, unafanya—unafanya nini, Ndugu Branham? Unakaa kwenye kundi la watu ambao ni makundi madogo tu *hapa* na *pale*.”

<sup>29</sup> Nikasema, “Sikiza, Mungu, wakati Yesu alipokuja, Yeye kamwe hakufikia vituo mhimu, alikuja kwa Wateule, huduma yangu ni kwa Wateule.” Nikasema, “Nifanyalo, nimeongozwa kulifanya, wala sijali kuhusu vituo muhimu, mimi huenda mahali Bwana aniongozapo.”

<sup>30</sup> Vipi kama nilikuwa na mipango mikubwa mno na ilinibidi kuwa na dola elfu *kadhaa* kila siku, ningefanya nini? Nisingekuwa na wasiwasi huo, ninamfurahia Bwana, Yeye alijua kutoniwekea hizo, sina nguvu za kutosha za kiakili kushughulikia hilo.

<sup>31</sup> Nikasema, “Ni—ni—nisingekuwa na vipindi hivi. Hainibidi kuwa na chochote.” Mnaona? Yote tu ninayohitaji ni neema Yake, hivyo tu. Hiyo ni kweli. Hiyo tu ndiyo ninayohitaji.

<sup>32</sup> Nilikuwa nimesimama si muda mrefu uliopita na kuangalia jengo kubwa, zuri lililokuwa limejengwa. Nami nikasimama pale na moyo wangu ukalia tu, ndipo nikawazia, “Loo, jamani, Bwana!” Nami nikaenda kule na kuangalia, Niliona jambo ambalo ndugu fulani walikuwa wamefanya, nikaangalia chini kule na kuona vitu hivi vikuu. Nami nikasimama huko nje na, kwa kweli, nitakiri hilo, watu wa ajabu, naam, bwana, watumishi halisi wa Kristo, nami nikawazia, “Jamani, si ni ajabu Bwana, lakini nina shida gani?” Mnaona? Nami nikasema, “Labda siwezi kuaminiwa.”

Mara nikasikia Sauti, ikasema, “Lakini Mimi ndimi Urithi wako.”

Nikasema, “Asante, Bwana, nitachukua tu sehemu hiyo.”

<sup>33</sup> “Mimi ndimi Urithi wako.” Ninapenda tu... Yeye anatak... Yeye ndiye Urithi wangu, huo ndio ninaotaka, Yeye awe Urithi wangu.

<sup>34</sup> Ninaamini Bwana yuaja karibuni, ninahubiri hilo, ninaishi hilo, ninataka kuamini hilo na kudumu nalo. Hiyo ni kweli. Na kama ukihubiri na kusema, “Bwana yuaja upesi,” na—na kufanya mambo, inaonekana kana kwamba itakuwa miaka milioni moja bado kabla hajaja, vema, matendo yako mwenyewe yanahukumu ushuhuda wako. Unaona? Hilo—hilo... Kama Yeye yuaja upesi, na tujiweke tayari. Hebu... .

<sup>35</sup> Jinsi Pentekoste hiyo ilivyo tofauti siku hizi na ilivyokuwa! Nilikuwa nikishirikiana na Wafanyabiashara Wakristo wa Full Gospel, kundi zuri sana, hilo ndilo shirika pekee nililo mshiriki wake, wala si dhehebu, ni kundi hai. Na sababu ya mimi kufanya hivyo, ninafanya wafanyabiashara kutoka katika kila kundi watoke, na—na halafu kidogo inamwaibisha mchungaji wao, maana watashirikiana, kwa hiyo basi, wanalileta kanisa lote, nami ninapata fursa ya kuwashughulikia wote. Ni—ninasimama katikati ya pengo na kusema, “Sisi ni ndugu, sisi ni ndugu. Hatupaswi kuwa na tofauti na mipaka, inatupasa kuwa ndugu, sote pamoja.”

<sup>36</sup> Nami nilikuwa huko Kingston, Jamaika, nami nilikuwa nimewasikia baadhi ya wafanyabiashara siku hiyo wakitoa ushuhuda mbele ya hao wafanyabiashara kule kuhusu, “Biashara yangu ndogo ilikuwa tu *hivi-na-hivi*, basi Mungu abarikiwe, nina Kadilaki tatu, pia nina *hiki, kile*, na *kinginecho*.”

<sup>37</sup> Usiku huo nilisema, “Loo, ndugu, jinsi Pentekoste ilivyo tofauti sasa na wakati huo wakati ilikuwa... wakati ilipoanguka kwa mara ya kwanza! Wakati ilipoanguka kwa mara ya kwanza,” nikasema, “hao watu waliuza walichokuwa nacho wakawa fukara, ili kuipeleka Injili.” Nami nikasema, “Siku hizi wanajaribu kuwaambia hao wafanyabiashara... Wana biashara, wanajua la kufanya, wao, hayo siyo wanayotaka.

Hebu wajue upendo wa Mungu, huo ndio wanaojaribu kupata, sio jinsi ya kuboresha biashara yao. Mungu haahidi maisha rahisi. Yeye. . . Njia ye—yetu imeparuza na ni ngumu, na kama huko tayari kushika njia hiyo, usianze, kwa sababu kama kweli unamtumikia Mungu, utapitia njia ngumu, ninamaanisha.”

Wengine kupitia majini, na wengine kupitia mafuriko,  
Wengine kupitia majaribu mazito, lakini wote kupitia kwa Damu.

Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo anavyowaongoza watoto Wake.

<sup>38</sup> Kulikuwako na maskini mwinjilisti fulani, mwimbaji pamoja nasi kule, akasema, “Lakini Ndugu Branham,” akasema, “huo ndio wakati mmoja ambapo—ambapo wanafunzi walikosea.”

Nikasema, “Ati nini hiyo? Siamini wangefanya hivyo, walikuwa watu waliovuviwa.”

<sup>39</sup> Akasema, “Vema, hapo watu wote walipouza mali zao na kuiweka miguuni pa mitume,” kasema, “wakati mateso yalipotokea, hawakuwa na makazi yoyote ya kuyaendea, hawakuwa na mahali pa kurejea.” Akasema, “Ilionyesha walikosea.”

Nikasema, “Mungu hakosei, la, bwana.”

Akasema, “Vema, wao, kama wanalikuwa na makazi ya kuendea. . .”

<sup>40</sup> Nikasema, “Hivyo ndivyo Mungu alivyowataka wafanye. Walitawanyika kote, bila makazi, na kueneza Injili kote nchini.” Kwa sababu hawakuwa na mahali pa kwenda, hivyo ndivyo ilivyombidi Mungu kufanya.

<sup>41</sup> Loo, laiti tungefuata mwongozo wa Roho, mnaona, basi ingekuwa ni afadhali kama tungerudi tu kwenye uongozi wa Roho na kuufuata huo, nasi tungekuwa bora zaidi, naamini.

<sup>42</sup> Sasa, tunatumaini sasa ya kwamba kila mtu ataponywa. Usiku wa jana ulikuwa usiku mtukufu. Ninahisi tu nguvu za Roho, jinsi alivyotenda kazi juu ya watu, na jinsi Mungu alivyotenda.

<sup>43</sup> Sasa, wachungaji, ndugu zangu, kumbukeni muda mrefu baada ya mimi kuondoka, nikiisha kuondoka hapa, kumbukeni kutakuwako na wanawake na wanaume ambao wamekuwa na matatizo kwa muda mrefu watakaokuja wakishuhudia, “Yamekwisha.”

<sup>44</sup> Jana usiku nikiondoka jukwaani niliyumbayumba, nisingeweza kujizuia. Mnaona? Ilikuwa vigumu kwangu kujua mahali nilipokuwa. Ilikuwa ni ongezeko kubwa sana la imani, mnaona, inaongezeka.

<sup>45</sup> Sasa, ni vibaya sana kwamba inatubidi tu kukaa siku chache tu kisha tuondoke. Mnaona? Laiti tungalingoja kidogo, laiti tungalikuwa na wakati! Lakini tunazurura tu kote nchini, kila mahali tuwezapo (Tukijaribu kuingia ndani ya, kila kiboko tunachoweza kumcharaza Shetani.), na kwa Kanisa teule, na kuwaacha waone ishara hiyo ambayo Kristo alisema ingekuwako kabla ya kule Kuja, kwa sababu sijui ni saa gani huenda akatokea, nami ninataka kufanya kila kitu kilicho katika uwezo wangu. Kwa hiyo niombeeni, hilo ndilo jambo bora zaidi mnaloweza kunifanyia, ni kuniombea.

<sup>46</sup> Sasa, kama nilivyosema, sina mipango ya kuunga mkono, ama chochote kile, na kama ningekuwa nayo, basi nisingeweza kuwa hapa. Kama ningalikuwa na...Wengi wa ndugu walio na miradi mikubwa wanayopaswa kusaidia, redio, televisheni ya ulimwenguni kote, na mambo makuu kama hayo, ha—hawangeweza kuhudhuria kundi dogo la watu.

<sup>47</sup> Lakini mnaona, Bwana alijua kidogo nilikuwa jamaa mdogo, vema, asiye na elimu, kwa hiyo angeweza kuniruhusu tu nishuke niwashike hao ambao hao ndugu wengine hawawashiki, nadhani. Nami nilifanya mkutano, hivi majuzi tu, katika kanisa lililoketi watu ishirini. Najua lilikuwa la kusikitisha, lakini niliufanya.

<sup>48</sup> Lakini kwa hiyo, mnaona, wakati Bwana anaponitaka niende ng'ambo, wasema, "Unafanyaje hilo?" *Kwa namna fulani* mtu fulani anakuja na kunipa pesa niende. Na kwa hiyo, basi kama itanibidi kwenda mahali padogo, sina masharti yoyote, ila kwamba naweza kwenda. Kwa hiyo ninaninii tu, mahali anaponitaka niende, Yeye hunishughulikia, nami ninaishi tu kwa imani, na kutembea kwa imani, na ambapo Yeye, chochote kile, kile anachotaka nifanye, Yeye daima huandaa njia.

<sup>49</sup> Nimewahubiria watu laki tano kwa wakati mmoja, pia nimewahubiria—nimewahubiria watano ama sita kwa wakati mmoja, nikafanya mkutano ambapo kumi au kumi na watano wangukuwa wameketi. Na baadhi ya mikutano mizuri sana niliyopata kuwa nayo ilikuwa katika m—mkutano wa maombi nyumbani, mahali fulani. Hiyo ni kweli. Mungu anaweza kuja kwenye kundi dogo ama kundi kubwa, ukubwa hauleti tofauti kwa Mungu, "Walipo wawili au watatu wamekusanyika, nitakuwa katikati yao." Jambo ndilo hilo.

Sasa, kabla hatujalikaribia Neno, tunataka kumwendea Mwandishi wake.

<sup>50</sup> Kuna mtu aliyewahi kumjua Booth-Clibborn? Wengi wenu nadhani. William Booth-Clibborn, aliandika ule wimbo maarufu, *Kushuka Kutoka Utukufuni Mwake*, yeye ni rafiki yangu binafsi. Naye anahubiri Injili katika lugha saba mbalimbali, yeye ni mwerevu tu sana. Huyu ni mjukuu wa mzee Jemadari Booth, naye ni Mwingereza. Na—naye, Booth,

huenda ameketi hapa. Kwa hiyo, yeye ni jamaa kwelikweli, mwanatheolojia halisi.

<sup>51</sup> Basi siku moja, kwa namna fulani tulibishania *jambo fulani*, na kwa hiyo, nikasema, “Vema, Ndugu Booth, hilo lingeweza kuwa, kwa kuwa *hili ni lile?*”

<sup>52</sup> Na sasa, Ndugu Booth, kama upo hapa, sikusudii kuifufua mada hiyo tena. Lakini alikuwa amefungwa, wala asingeweza kuwa na mahali pa kwenda. Kwa hiyo yeye alininii tu... Nilimwacha tu aruke, mpaka akaruka moja kwa moja kwenye mtego wake mwenyewe. Mnajua, kama tu, mpe ng’ombe kamba ya kutosha naye atajinyonga. Kwa hiyo, akafikia mwishoni mwa tawi wala asingeweza kurudi. Nami nikasema, “Vipi sasa, Ndugu Booth?”

Akasema, “Huijui tu Biblia yako.”

Nikasema, “Ila ninamjua Mwandishi wake vizuri sana.” Nikasema (Ndivyo hivyo.), kisha nikasema, “Yeye atanifundisha yaliyosalia.”

<sup>53</sup> Kwa hiyo, kama hatujui Neno, hebu na tumjue Mwandishi wake vizuri sana. Naye hatatuacha twende kombo, atatuongoza, kwa namna fulani, kwenye haki. Kwa hiyo, hebu na tuzungumze Naye sasa, kabla hatujalikaribia Neno Lake, tunapoinamisha vichwa vyetu.

<sup>54</sup> Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru kwa ajili ya fursa hiyo tena, upande huu wa Umilele, kumleta Yesu Kristo mbele ya kusanyiko linalongojea.

<sup>55</sup> Na sasa, mara nyingi nimewazia jinsi, kile ningefanya kama ningekuwa na—na sinia, ama, bilauri mkononi mwangu, na ndani ya bilauri hiyo mlikuwamo tone moja la Damu halisi ya Yesu. Jinsi ningekumbatia hiyo kwenye moyo wangu! Na jinsi ibada ambazo ningekuwa nazo kwa ajili ya hilo zingemiminika, huku machozi yakitiririka shavuni mwangu, kwamba nimeshika mkononi mwangu tone moja la Damu halisi ya Bwana Yesu, ile Damu Ambayo iliniokoa!

<sup>56</sup> Na huko ng’ambo wakati madaktari waliponipa dakika tatu tu za kuishi, zaidi ya miaka thelathini iliyopita, iliniokoa na kuniponya. Ee Mungu, jinsi ambavyo nimekuona Wewe, kote katika miaka, ukichukua makumi elfu mara maelfu ya wagonjwa ambao matabibu wetu walikuwa wamewakatia tamaa, na kuwafanya watu wenye afya na wazima kuendelea na maisha yao, hiyo Damu ndiyo iliyofanya hilo. Nami ningewazia jinsi ningeshikilia hiyo!

<sup>57</sup> Lakini, usiku wa leo, katika Neno Lako Mwenyewe ninashikilia zaidi ya tone moja la hiyo Damu, ninashikilia mbele zangu wale walionunuliwa kwa Damu hiyo. Yeye aliwapenda watu Wake kuliko alivyoyapenda maisha Yake Mwenyewe, kwa hiyo akatoa Damu ya uhai Wake kuwanunua watu hawa. Basi,

Bwana, niwaendeje? walio wakubwa kuliko ile Damu yenyewe, gharama ya Damu iliyonunuliwa.

<sup>58</sup> Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba utanificha nisije nikawaona watu, wala kuwaogopa watu, wala chochote kile, bali kulihubiri tu Neno, kuliweka wazi na dhahiri. Ndipo basi naomba Wewe uje nyuma ya hayo na kuthibitisha yale niliyosema kwamba ni kweli, na ndipo hilo linalifanya kweli, Bwana. Na iwapo kamwe sitakutana na watu hawa tena upande huu wa Mbingu, ama, upande huu wa Hukumu, basi hakutakuwa na damu ya mtu yeyote mikononi mwangu, Bwana, Nawe utakuwa huru kwa sababu unathibitisha Neno Lako. Ninaomba utatujalia, usiku wa leo.

<sup>59</sup> Waponye wagonjwa, Bwana, na uwaokoe wale wanaoweza kuokoka, wote uliowaita, kama kuna yeyote wa hao humu ndani usiku wa leo, Bwana, ambaye kabla ulimwengu haujaanza, kwamba kwa kujua Kwako kukuu tangu zamani ulijua wataokoka, na usiku wa leo, kwa namna fulani, umewaingiza moja kwa moja mahali hapa. Jalia jambo fulani lifanywe, usiku wa leo, ambalo litawafanya wamtambue Mwokozi wao mpendwa, na kumpokea. Ninaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>60</sup> Sasa, katika maandishi ya Mathayo Mtakatifu mlango wa 14 na kifungu cha 27:

*Mara Yesu akasema nao, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msiogope.*

<sup>61</sup> Ninataka kutumia neno hilo la *Msiogope*. *Msiogope*, [Kiingereza: Be Not Afraid—Mfa.] maneno matatu kwa ajili ya somo.

<sup>62</sup> Ndipo basi, hapana shaka ilikuwa karibu wakati jua lilipokuwa likitua, siku ndefu, yenye uchovu, iliyojikokota, mambo mengi yalikuwa yametukia, nami ninaweza kuona hiyo misuli mikubwa ikivimba chini ya mabega yake, alipoanza kuhamisha mtumbwi huo kutoka kwenye fuo za Galilaya zilizojaa mchanga na kuusukuma majini. Yule mvuvi mkubwa shupavu, aliyeitwa Simoni basi akachukua mahali pake alipokuwa akipitia kwenye ile meli ndogo, akaketi karibu na ndugu yake, Andrea, akatwaa kasia.

<sup>63</sup> Basi hiyo meli ndogo ilipoanza kusogea majini polepole, mayowe ya watu kutoka ukingoni, walikuwa wakipiga mayowe, “Rudini mkatuone tena. Tunathamini sana nyinyi kututembelea.” Jinsi mioyo yao hapana shaka ilifurika kujua ya kwamba walikuwa wamefanya jambo lililokuwa jema! Sisi sote tunapenda kusikia hilo, loo, kila mtu. Wakati mwingine kuondoka kwenye mkutano, watu wanalia tu.

<sup>64</sup> Na hapa, nilipokuwa nikiondoka Afrika Kusini, hivi majuzi, kulikuwa na yapata watu elfu kumi kwenye uwanja wa ndege, nao walikuwa huko nje, wamesimama huko nje wakitokwa machozi, na kulia, wakipiga nduru, wakipiga mayowe, “Rudini

tena mkatwambie tena habari za Yesu,” mnaona. Mambo mengi sana makuu!

<sup>65</sup> Ndipo maskini daktari aliyekuwa ameaona mwujiza ukifanywa, maskini mvulana mwenye mkengeza akaelekea jukwaani, mwenye mkengeza tu kadiri alivyoweza kuwa, na kabla hajanifikia macho yake yakawa sawa. Wakamwondosha tu jukwaani, ndipo daktari Mwingereza akarudi kutoka kwenye . . . akiketi huko nyuma, naye akaja, kasema, “Ulimfanyia nini mvulana huyo? Je, ulimpumbaza akili?”

Nikasema, “Ati kumpumbaza akili?” Nikasema, “Na wanakupa leseni ya kutibu, huku unajua zaidi kuhusu upumbazaji akili kuliko *huo*?”

<sup>66</sup> Naye akasema, “Mimi nilimweka mvulana huyo jukwaani alikuwa na mkengeza, naye huyu hapa, macho yake yamenyoka.” Kasema, “Jambo fulani lilitukia kati ya *pale* na *pale*.”

Nikasema, “Alikutana na Yesu.” Mnaona?

Nami nikasema, “Sikumgusa kamwe.”

Naye akasema, “Je, ulimpumbaza akili?”

<sup>67</sup> Nikasema, “Hakika sivyoy, bwana.” Nikasema, “Iwapo kupumbaza akili kutayanyosha macho yenye mkengeza, si afadhali ninyi jamaa mwanze mazoezi ya upumbazaji akili?” mnaona. “Ingekuwa bora kuliko upasuaji wowote mngaliweza kufanya, kama kupumbaza akili kutafanya hivyo.”

Nikasema, “La, sikumpumbaza akili mvulana huyo, Mungu aliyanyosha macho yake.”

<sup>68</sup> Akasema, “Na—najua kuna Mungu,” akasema, “najua kuna Mungu.” Kasema, “Hi—hi—hilo yungiyungi . . .” Mayungiyungi yao kule, kina dada, kama huenda mnajua baadhi yao, mbona, hayo mayungiyungi makubwa ya kala yana upana wa inchi kumi na nane, makubwa ya manjano na meupe, kitu kizuri kuliko vyote, kikikulia chenyewe moja kwa moja msituni. Walikuwa na mashada yake makubwa yamewekwa kila mahali kwenye jukwaa. Kasema, “Ninajua kuna Mungu, uhai ndani ya hayo mayungiyungi, kwa sababu yungiyungi lisingeweza kuishi bila uhai.” Akasema, “Lakini wa kushikika vya kutosha kufanya upasuaji wa macho hayo?”

Nikasema, “Kwanza ni nani aliyeumba macho?” Mnaona? “Yalitoka wapi?”

Naye akasema, “Vema . . .”

<sup>69</sup> Na papo hapo, Dk. Bosworth akaja na kusema, “Itakubidi kuondoka, bwana, utasababisha ghasia. Unaona?” Kasema kwamba “Wakati ni muhimu sana sasa, wakati huo upako ukiwa juu ya ndugu yetu.” Kasema . . .

<sup>70</sup> Kwa kawaida tunapokuja mikutanoni, kuifanya ifanikiwe zaidi, Bw. Baxter na Bw. Bosworth na hao wengine, ma—mameneja, wao ndio wanaozungumza, ninakuja tu moja kwa moja, moja kwa moja jukwaani, ninaitisha mstari wa maombi, kisha baada ya kumalizika, ninaondoka. Na, lakini sasa, bila shaka niko tu hapa peke yangu pamoja na hawa wavulana, na kwa hiyo ninaninii, ninajaribu kutapatapa kote katika kuzungumza, mimi mwenyewe.

<sup>71</sup> Kwa hiyo basi, wakati da—daktari... Naye akaanza kumwondosha. Ndipo akasema, kisha akasema, “Hebu kidogo,” akasema, “Bw. Branham, unataka kuniambia ya kwamba Mungu, yule Muumba mkuu, yuko mahali fulani kati ya *hapa* na *pale*?”

Nikasema, “Yuko kila mahali.”

Naye akasema, “Mimi... Vema, hapana shaka kuna Nguvu fulani dhahiri, zilizoyanyosha macho ya mvulana huyo.”

Nami nikasema, “Ilikuwa ni Mungu.”

<sup>72</sup> Nao wakaanza kumwondoa, ndipo Bw. Baxter akamwendea. Akasema, “Hebu kidogo.” Akafika kwenye, kwenye maikrofoni, akasema, “Mimi, pia, nitampokea Yesu Kristo kama Mwokozi wangu binafsi.”

<sup>73</sup> Ndipo nilipokuwa nikiondoka Johannesburg, hii ni kweli, Mungu aliye Mbinguni anajua, basi nilipokuwa nikiondoka Johannesburg, aliruka ua, mahali walipokuwa wamemweka huko nyuma, akakimbia huko nje na kunikumbatia kwa mikono yake nilipotoka miongoni mwa watu, na walinzi, tukienda kwenye Shirika la Ndege la Pan American. Nilipoenda huko nje, wao... alikimbia huko nje na kunikumbatia kwa mikono yake, na kusema, “Bwana ameniita kwenye huduma.” Hakuwa na... Akaanza kunena kwa lugha, huku ameikumbatia shingo yangu, namna hiyo, hivyo, daktari Mwingereza.

<sup>74</sup> Kwa hiyo sasa, nilisikia kutoka kwake, hapa yapata miaka miwili ama mitatu iliyopita, yapata miaka miwili iliyopita. Imekuwa kama miaka mitano iliyopita. Yeye ana huduma kubwa huko juu, akiwasaidia, kweli, wagonjwa na wanaoteseke huko Afrika.

<sup>75</sup> Kwa hiyo, wakati watu wakipunga mkono, “Kwaheri, rudi tena,” hilo linaufanya tu moyo wako kujisikia vizuri sana. Na ni jambo unalojua kwamba unahisi kwamba umetimiza jambo fulani. Nao wanafunzi hawa hapana shaka walijisikia hivyo wakati wote walipokuwa wakiwapungia mkono wa kwaheri, “Tutawaona tena, na mrudi nchini mwetu tena, na—na kuzungumza nasi tena.”

<sup>76</sup> Basi wakati jua lilipokuwa likishuka chini, na meli hiyo ndogo ikishika njia, na kila mmoja wa hao wavuvi, na mabaharia wakivuta hayo makasia makubwa, huku wao... .

<sup>77</sup> Meli siku hizo, zilikuwa—zilikuwa na makasia, mawili, moja upande *huu* wa kiti, na moja upande *ule*. Nao wangeketi pamoja na makasia makubwa na kudumisha tu wakati huku wa—wakipiga meli makasia.

<sup>78</sup> Nayo inapitia kwenye maji matulivu, ndipo, hatimaye, wakafikia umbali wa kutoweza kusikiwa na watu waliokuwa wamesimama ukingoni wakipunga mikono. Na hapana shaka waliendelea kuvuta, labda, kwa dakika zingine kumi na tano, ishirini, ama thelathini. Nami sijui, hapana shaka ilikuwa ni kijana Yohana, alikuwa ndiye mdogo wa kundi hilo, na mtu aliyekuwa ndani usiku huo, melini, hapana shaka alisimama apate kupumua, maana walikuwa wakivuta kwa nguvu sana, iliwabidi kuvuka bahari usiku huo, ama, maskini hilo ziwa.

<sup>79</sup> Basi akasimama, labda, na kuziondoa nywele zake machoni mwake na kusema, “*Whiu!*” walipopata pumzi, na kusema, “Ndugu,” hakuna mtu aliyekuwa amesema kitu kwa muda mrefu sana, kasema, “Mimi . . . jambo moja leo, sote tunaweza kuwa na hakika kabisa ya kwamba hatumfuati mdanganyifu, kama vile watu wanavyodhani ndivyo alivyo.”

<sup>80</sup> Kasema, “Mnajua, wakati mvulana huyo mdogo alipokuja pale na hizo biskuti tano ndogo, samaki wawili, na kumkabidhi Yeye, nami nikashangaa atafanya nini nazo. Ndipo nilipomwona akiumeza mkate huo na kutukabidhi, nilipanda nyuma Yake nione mahali hiyo ilikuwa ikitoka. Lakini akachukua biskuti, akaivunja tu, akaiweka kwenye trei, na kufikia wakati aliponyosha mkono tena, kulikuwa na biskuti nyingine, akaivunja. Akawachukua samaki hao . . .”

<sup>81</sup> Sijui aliachilia atomi ya namna gani basi, ndugu, sijui alilofanya. Si samaki tu, bali samaki waliopikwa; sio unga tu, lakini unga uliookwa, tayari katika mkate. Yeye aliachilia kitu gani? Akaviweka juu ya sahani hizo zenye biskuti tano na samaki wawili, na kuwalisha watu elfu tano, na kuokota vikapu vilivyojaa vipande vilivyosalia. Yeye alifanya nini?

<sup>82</sup> Ninaweza kumsikia kijana Yohana akisema, “Nilimwona katika mambo mengi makuu, daima nimemwamini, lakini leo hii hilo lilitosha. Ninakumbuka nilipokuwa mvulana mdogo wa Kiyahudi, mama yangu alikuwa akiniweka pajani mwake, naye angeniambia, ‘Yohana?’ Nami ningeyaangalia macho yake makubwa, ya kupendeza, ya hudhurungi, naye angesema, ‘Yohana, nataka kukusimulia hadithi za Biblia.’ Na jinsi nilivyokuwa nikizipenda!”

<sup>83</sup> Ni vibaya sana kwamba akina mama hawawachukui watoto wao siku hizi na kuwasimulia hadithi za Biblia. Ni vigumu kumpata mchungaji ambaye atafanya hivyo, sembuse ma—ma—mama. Nafikiri kuna—kuna Injili tano, mnajua tu nne katika Biblia, bali ni Mathayo, Marko, Luka, Yohana, na Mama. Mama huwachukua wangali wachanga, anapaswa kuanza nao papo

hapo kabla hawajajua lolote kuhusu Mathayo, Marko, Luka, na Yohana.

<sup>84</sup> Laiti akina mama wangetumia muda mwingi zaidi kuzungumza na watoto wao habari za Mungu na kuwaombea, tungekuwa na kupungua kwa uhalifu wa vijana. Kwanza kabisa, ni uhalifu wa wazazi kabla hatujawa na uhalifu wa vijana. Kama akina mama wangechukua mahali pao nyumbani, na Biblia, na kuwaombea watoto wao, na kuwaongoza kwa Kristo, badala ya kutoka kwenda kwenye karamu ya kushona na kucheza karata, na kunywa pombe, na kufanya yasiyofaa, na kuvuta sigara na... Vema, sitaki kuingilia jambo hilo. Lakini, hata hivyo, mimi... Inatisha jinsi mambo yanavyoendelea.

<sup>85</sup> Leo nilimcheka maskini mke wangu. Tulikuwa kwa Howard Johnson kununua moja ya hizo 3-D. Mnajua hiyo ni, kwa kawaida mimi sili sana wakati wa ibada za namna hii. Nasi tulikuwa huko juu, naye akamwona nanii, mama mmoja huko juu aliyekuwa amejipaka hii hapa *rangi ya makucha*, mwajua, chochote ulicho upuuzi huo.

<sup>86</sup> Na yapata majuma mawili yaliyopita, nilikuwa California, sikujua tayari mambo yamepotoka umbali huu, nami nilikuwa nimesimama kwenye Mkahawa wa Clifton, nami, nikimngojea Ndugu Arganbright, ambaye ni Makamu wa Rais wa Wafanyabiashara wa Full Gospel, nami nilipaswa kukutana naye hapo, ndipo msichana mmoja akaingia mahali hapo, nami nikamwangalia, ndipo nikawaza, "Vema, maskini mama huyo!" Sasa, macho yake yalikuwa kitu cha kuchukiza sana. Nikawaza, "Yeye ni mgonjwa, nitaenda pale nikamwombee." Nami ni—nilikuwa nimeona, nimeona ophthalmia, na nimeona glakoma, nimeona ukoma, ila sijawahi kuona kitu kama hicho. Nami nikawazia, "Yeye..." Kwa kweli, ni—ninasema kweli, nilifikiri msichana huyo alikuwa kitu fulani, ugonjwa ambao sijawahi kuuona hapo kabla. Kwa hiyo yeye, macho yake yalikuwa ya kijani kibichi sana, halafu bluu kabisa nyuma ya hiyo.

<sup>87</sup> Ndipo nikawaza, "Mimi... Huyo mtoto, yukoje hapa nje mtaani namna hiyo?" Nami nikawazia ningemwendea na kusema, "Dada, samahani, mimi ni mhudumu wa Injili. Macho yako yana shida gani? Je, naweza—naweza kukuombea dua kidogo, kama daktari hajui? Labda..."

<sup>88</sup> Nami, mara nilipoanza kumwendea, hawa hapa wanawake wengine wanakuja na kitu kile kile, nami nikawazia, "Sijui kama hiyo ni namna fulani ya *rangi ya makucha* wanayojipaka machoni mwao," mwajua. Na—nao, ikiwafanya...

Ndipo basi ni—nikamwuliza mtu mwingine, nao wakasema, "Naam, hi—hicho ni kitu wanachopaka usoni mwao."

<sup>89</sup> Nami, nilipokuja nyumbani, nilimwambia mke wangu kuhusu hilo, basi nikasema, "Mpenzi, hata hawakuonekana kama wanadamu. Unaona? Ilionekana kama kitu kilichotoka

kwenye sayari nyingine, ama—ama kilichoanguka kutoka kwenye chumba cha maiti mahali fulani, ama kitu fulani.” Nikasema, “Sijawahi kuona kitu kama hicho!”

<sup>90</sup> Na leo hii, tulikuwa huko juu, na pale aliketi mama mmoja kama huyo, ndi—ndipo Meda akaangalia huku na huku, mke wangu, naye akasema, “Hicho *ndicho* Bill?”

Nikasema, “Ndicho hicho.”

Akasema, “Jamani, huyo si angekutisha usiku?”

Nikasema, “Ingenitia—ingenitia baridi na homa.” Hakika ingenitia.

Naye akasema, “Vema, mbona hivyo?”

<sup>91</sup> Tuliuliza si muda mrefu uliopita, niliona jambo la ajabu mjini mwetu, mama fulani alikuwa amevaa sketi, nami nikasema, “Si ni ajabu hii? Si anaonekana mzuri?”

“Naam, hakika ni mzuri.” Akasema, “Bill, huyo, hao wanawake, ninajua baadhi yao huimba katika kwaya, na kadhalika.”

Nikasema, “Hakika.”

Akasema, “Vema, kuhusu sisi,” akasema, “ni kitu gani kinacholeta tofauti?”

<sup>92</sup> Nikasema, “Vema, mpenzi, hao ni Wamarekani tu, unaona, hivyo tu ndivyo walivyo. Unapokuwa Ujerumani, wana roho ya Kijerumani huko Ujerumani; ukienda Ufini, wana roho ya Kifini; ukienda Ufaransa, wana roho ya Ufaransa; ukija Marekani, una roho ya Kimarekani.”

Akasema, “Kwani sisi si Wamarekani?”

<sup>93</sup> Nikasema, “Loo, la, bila shaka sivyo, tungalikuwa Wamarekani, tungetenda kama Wamarekani. Unaona?” Nikasema, “Hao ni Wamarekani, kwa hiyo hayo ndiyo yote wajuayo, wanajiunga na kanisa mahali fulani, lakini ninii tu, wao ni wa duniani tu, na hayo tu ndiyo yote wajuayo.” Yeye. . . Nikasema, “Sasa, ona. . .”

Akasema, “Kwani tumetoka wapi?”

Nikasema, “Kutoka juu, ndipo tunatenda kana kwamba tumetoka huko juu. Unaona? Wanawake wetu wanavaa kana kwamba wametoka huko juu. Mnaona? Wa—wa wanatenda hivyo. Wao. . .”

<sup>94</sup> Sisi ni Wakristo, tumezaliwa mara ya pili, Ufalme wetu unatoka juu, kutoka Mbinguni. Tumezaliwa kwa Roho atokaye huko juu, kwa hiyo tunatenda kana kwamba tumetoka huko juu, ambamo wanaishi watakatifu, na wenye haki, na waaminifu, na wanyofu wao kwa wao, kumtendea mema kila mtu, na kufanya yote wawezayo kusaidiana, si hapa chini katika mkusanyiko wa namna hii.

<sup>95</sup> Kwa sababu tu wewe ni Mmarekani, hilo halikufanyi Mkristo. Bw. Bosworth wakati mmoja jukwaani alimwuliza msichana mmoja, kasema, “Je, wewe ni Mkristo?”

<sup>96</sup> Akasema, “Nitakufahamisha mimi huwasha mshumaa kila usiku.” Kana kwamba hilo lilikuwa na uhusiano wowote na Ukristo! Lakini hivyo ndivyo ilivyo. Mnaona?

<sup>97</sup> Loo, laiti tungechukua tu wakati zaidi kuwasimulia watoto wetu hadithi za Biblia! Ninawazia ningeweza kwenda kwenye mji huu na kumchukua kila mvulana mdogo katika mji huu, na kila mmoja wao anaweza kuniambia Davy Crockett alikuwa ni nani, nami ninaweka dau ha—ha—hakuna ishirini kati ya mia moja wanaoweza kuniambia Yesu Kristo alikuwa ni Nani, na wakati alipozaliwa. Hiyo ni kweli. Loo, hakika. Mnaona, hiyo ni—ni roho tu ya Kimarekani ikipita, hivyo tu, mnaona.

<sup>98</sup> Na sasa, tunaona ya kwamba, leo, hiyo ni kusema, tumepanda upepo na tunavuna tufani, hivyo ndivyo tu tunavyofanya hasa. Sasa, lakini tunapaswa kuwa tukiwafundisha watoto wetu kuhusu Kristo.

<sup>99</sup> Maskini Yohana, mama yake alikuwa amemfundisha habari za Mungu, naye akasema . . .

<sup>100</sup> Mwajua, angalieni, wakati jambo hilo linapokuja, wakati jambo hilo litakapotimia, mtoto aliyefunzwa vizuri, “Mlee mtoto katika njia impasayo, naye atakapokuwa mzima, hataiacha.”

<sup>101</sup> Sasa, tunaona ya kwamba, akimlea mtoto huyu, alikuwa amemlea Yohana vizuri, “Akasema, ‘Yohana,’ naye angekumbuka hiyo hadithi, “kasema, ‘Jinsi ambavyo Yehova, jinsi alivyowashughulikia watu Wake, wakati wote walipokuwa kwa nia moja, na kuifuata ile Nguzo kuu ya Moto,’ na kusema, ‘Yohana, mwanangu, siku moja wakati Mungu alipowatoa watu Wake kutoka utumwani, Yeye aliwapeleka huko nyikani, nawe unajua, Yohana, kila asubuhi wangetoka na kuokota mkate wenye asali juu yake, biskuti za asali.”

<sup>102</sup> Na sasa, yeye akasema, “Mama, hivi Mungu ana lundo la majiko huko juu Mbinguni? Na ana Malaika wengi wanaooka mkate huu kila usiku na wangeumwaga chini?”

<sup>103</sup> “‘La, Mpenzi,’ akasema, ‘Mungu hana majiko angani. Unaona, Mungu ni Muumba, na yote anayopaswa kufanya ni kunena tu, Naye huumba vitu kutokana na vitu ambavyo hakuna kitu cha kuviumbia, ama, hakuna kitu cha kuviumba, unaona. Yeye tu, Yeye ni Muumba.’”

<sup>104</sup> Ndipo Yohana akasema, “Ndugu, leo, nilipomwona amesimama pale na kuchukua mkate na kuumba mkate, nilijua hapana shaka ana uhusiano fulani na Yehova. Kwa hiyo tunajua ya kwamba Mtu tunayemfuata, ingawa makanisa yanasema ya kwamba Yeye ni laghai, Yeye ni mpiga ramli, Beelzebuli, lakini ninajua ya kwamba Yeye ni Yehova, kwa sababu Yeye hutenda

kama Yehova, Naye hufanya mambo ambayo Yehova hufanya, kwa hiyo tunajua ya kwamba lazima iwe ni Yehova.”

<sup>105</sup> Sasa, siku hizi watu wengine hata hawaamini hilo, watu wengine wanataka kumfanya Yesu mtu wa kawaida tu, mtu mwema. Wakati fulani uliopita, mwanamke wa dhehebu fulani na kanisa ambalo haliamini kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, aliniambia, akasema, “Ndugu Branham, ninathamini mahubiri yako, lakini,” kasema, “unatilia mkazo sana Kristo kuwa ni Mungu,” kasema, “hakuwa Mungu, alikuwa ni mwanadamu.”

Nikasema, “Lakini Yeye alikuwa ni Mungu.”

Akasema, “Loo, alikuwa ni mtu mzuri, naye alikuwa ni nabii.”

Nikasema, “Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii, Yeye alikuwa ni Mungu; chochote pungufu ya hayo, tumepotea.”

Naye akasema, “Loo, la, a—asingeweza kuwa Huyo.”

Nikasema, “Alikuwa Huyo.”

Basi akasema, “Ulisema ulikuwa wa kimsingi, nawe ulinena tu mahali Biblia inenapo, na kadhalika.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

Akasema, “Kama nitakuthibitishia kwa Biblia yako ya kwamba yeye hakuwa kitu ila mwanadamu, utaamini?”

Nikasema, “Kama Biblia ilisema hivyo, bali huwezi kuthibitisha hilo.” Unaona? “Lakini Biblia haisemi hivyo.”

<sup>106</sup> Akasema, “Vema, nitakuthibitishia.” Kasema, “Katika Yohana Mtakatifu mlango wa 11 kwenye kifo cha Lazaro, Biblia ilisema ya kwamba Yesu, akienda kaburini mwake, alilia.” Kisha kasema, “Unaona, hilo lilimfanya mwanadamu tu.

<sup>107</sup> “Vema,” nikasema, “hakika alilia.” Nikasema, “Lakini Yeye alikuwa zaidi ya mwanadamu,” nikasema, “huyo alikuwa ni Mwanadamu aliyekuwa akilia, bali Mungu alikuwa ndani Yake.”

Naye akasema, “Loo, la, asingeweza kulia na awe ni Mungu, kama unavyosema ndivyo alivyo.”

<sup>108</sup> Nikasema, “Basi ninataka kukuuliza jambo fulani. Nitakubali ya kwamba Yeye alilia alipoenda kwenye kaburi la Lazaro, lakini alipoyanyosha mabega Yake madogo, kasema, ‘Lazaro, njoo huku,’ na mtu aliyekuwa amekufa na yuko kaburini na tayari anaoza akafufuka, hiyo ilihitaji zaidi ya mwanadamu kufanya hivyo, Huyo alikuwa ni Mungu aliyefanya hivyo.” Naam, bwana.

<sup>109</sup> Nikasema, “Kweli, aliposhuka kutoka mlimani usiku huo na alikuwa na njaa, akiangalia, ama, siku hiyo alikuwa na njaa, akitafuta kitu cha kula kutoka kwenye hiyo mitini, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati aliposhikwa na njaa, lakini,” papa hapa, nilikuwa nikizungumza kuhusu, “wakati alipochukua hizo biskuti tano na samaki wawili, na

kuwavunja, na kuwalisha elfu tano, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa ni Mungu.” Hiyo ni kweli. Hakika.

<sup>110</sup> Alikuwa mwanadamu wakati alipokuwa amelala nje kwenye meli hiyo usiku huo, amechoka sana, nguvu zilikuwa zimemtoka kutokana na kuwaponya wagonjwa, alikuwa amechoka sana hata yale mawimbi makubwa, yenye nguvu hata hayakumwamsha, ambapo kuna...Mbona, nawazia maskini meli hiyo ilikuwa ikirushwarushwa huku na huku kama kifuniko cha chupa huko nje kwenye ile bahari kuu, pepo elfu kumi wa baharini waliapa wangemzamisha usiku huo. Alikuwa ni mwanadamu, amelala pale, amechoka, lakini mara alipoamshwa, aliweka mguu Wake kwenye demani ya chombo na kusema, “Amani, tulia,” ndipo pepo na mawimbi yakamtii, Huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, Huyo alikuwa ni Mungu.

<sup>111</sup> Alilia apate rehema msalabani kama mwanadamu, hiyo ni kweli, lakini kwenye asubuhi ya Pasaka wakati alipovunja mihuri ya mauti, akavingirisha kaburi, akafufuka, na kupaa Juu, ilikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Si ajabu nabii alisema, ama, mshairi alisema:

Alipoishi, alinipenda; akifa, aliniokoa;  
Alipozikwa, alizipeleka dhambi zangu mbali  
sana;  
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:  
Siku moja Yeye yuaja—loo, siku tukufu!

<sup>112</sup> Ameichangamsha mioyo ya wanadamu. Na kila mwanamume au mwanamke aliyepata kuwa na maana yoyote katika maisha haya, Abraham Lincoln, George Washington, yeyote yule, aliamini hilo, washairi wote kote katika miaka. Kipofu Fanny Crosby aliimba:

Usinipite, Ee Mwokozi mpole,  
Sikia kilio changu kinyenyekevu;  
Unapozuru wengine,  
Usinipite.  
Wewe uliye Kijito cha faraja yangu yote,  
Zaidi ya uhai kwangu,  
Ni nani niliye naye duniani ila Wewe?  
Au ni nani Mbinguni ila Wewe?

<sup>113</sup> Wakati Eddie Perronet, wakati asingeweza kuuza nyimbo zake, wala hakuna hata mmoja wao angemsikiliza, Mkristo aliye karibu na kufa, siku moja Roho Mtakatifu alimshukia, akanyakua kalamu na kuandika ule wimbo wa ushindi. Akaimba, akaandika wimbo:

Nyote zisifuni nguvu za Jina la Yesu!  
Malaika na wasujudu;  
Leteni taji ya kifalme,  
Na kumtawaza kuwa Bwana wa wote.

114 Amina. Amina. Loo, hakika, Yeye alikuwa zaidi ya mwanadamu, alikuwa Mungu. Hiyo ni kweli. Yeye hakuwa Myahudi wala Mmataifa, Yeye alikuwa ni Mungu. Seli hiyo ya Damu ilitokana na jinsia ya kiume ambayo ilikuwa ni Mungu. Mungu aliumba Chembe ya Damu katika tumbo la uzazi la bikira Mariamu, na kupitia Chembe hiyo ya Damu akatokea Mwana wa Mungu. Mungu aliishi mle ndani, Damu isiyoghoshiwa, hakuna kujuana kimwili kulikohusishwa nayo hata kidogo namna hiyo. Na kupitia Damu hiyo tunapewa imani kwenda kwa ujasiri kwenye kiti cha enzi cha Mungu na kudai ahadi yoyote iliyo katika Biblia hii, kwa sababu Mungu alitoa ahadi. Hiyo ni kweli. Naam.

115 Wale waabudu wa kale wa Agano la Kale walileta mwana-kondoo, wakaweka mikono yao juu yake, walichukua ndoana na kukata maskini koo lake, huku akirusha mateke, na kulia, na kufa, nayo damu ikinyunyizia mikononi mwa mwabuduo, alijua ya kwamba mwana-kondoo huyo alikuwa akifa mahali pake. Lakini alirudi akiwa na tamaa ile ile aliyokuwa nayo wakati alipoingia, kwa sababu uhai uliokuwa katika chembechembe hiyo ya damu ya mwana-kondoo ulikuwa ni uhai wa mnyama ambaye hakuwa na nafsi, kwa hiyo usingeweza kumrudia mwabuduo. Lakini sasa mwabuduo akiisha kusafishwa kwa Damu ya Kristo, hana tena dhamiri, au hana tena tamaa ya dhambi.

116 Wakati mtu, kwa imani, anapokuja kwenye Chemchemi hiyo iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, kwa imani, anapoweka mikono yake juu ya miguu ya Mwana wa Mungu na kuangalia pale Kalvari, na kujua mateso yote aliyofanya, Yeye alimfanyia, basi Seli hiyo ya Damu ilivunjwa pale Kalvari, haikuwa ni mnyama, wala haikuwa ni mwanadamu, ilikuwa ni Damu ya Mungu Mwenyewe ambayo inarudi na kutoa kuzaliwa upya. Roho huyo anayetoka mle, anaingia katika roho ya mwanadamu na kumfanya mwana ama binti wa Mungu. Amina. Huko ndiko kuzaliwa upya. Hiyo ndiyo Injili iwapo ninajua lolote kuhusu.

117 Ile Seli aliyokuwa mle ndani, Mungu alijiumba Mwenyewe pamoja na Nafsi Yake Mwenyewe, alishuka akaja akiwa Mtoto mchanga, Yehova, na akazaliwa kwenye zizi juu ya samadi, na—na linapaswa kuwa ni muhimu sana kwa watu, mtoto Yehova amelala, akilia katika zizi. Loo, jamani! Nasi tunafikiri sisi ni *mtu muhimu*, kwa sababu... Loo, jamani! Yehova akicheza kama mtoto, Yehova akifanya kazi kama mwanadamu, Yehova akifa kama mwanadamu, bali Yeye alikuwa ni Yehova wakati alipofufuka tena, alithibitisha alikuwa Yehova. Hakika, alikuwa hivyo. Naam, bwana. Naam.

118 Yohana alisema, “Nilijua ya kwamba Huyu alikuwa Ndiye, niliona mambo aliyofanya, ninajua ya kwamba hakuna kitu

chochote kingeweza kufanya hivyo ila Yehova.” Kasema, “Nimeridhika, ndugu. Nitaingiza ushuhuda wangu ndani.”

<sup>119</sup> Mnajua walikuwa na mkutano wa ushuhuda hapa nje baharini, hapo ni mahali pazuri pa kufanyia mmoja. Kila mtu, mnajua wakati kila mtu anaposhuhudia, vema, kwa kawaida Bwana hushuka na kuwabariki, mwajua. Kwa hiyo walikuwa na mkutano wa ushuhuda, wakati wakingojea, wakisafiri. Laiti tungalikuwa na mmoja, usiku wa leo, tutatoa mkutano wa ushuhuda hapa. Hebu na tuusikilize wao kwa dakika chache, wanaposafiri. Nawe katika gome lako dogo, unapoabiri bahari adhimu ya maisha:

Shuhudia, imba, au omba,  
Na kama mkate juu ya maji,  
Utakurudia siku moja.

Nena neno dogo kwa ajili ya Yesu, (Fanya jambo fulani.)  
Shuhudia, imba, au omba.

<sup>120</sup> Naam, mfanyie jambo fulani, tunaposafiri kwenye bahari adhimu ya maisha. “Ndugu mpweke na aliyepatwa na ajali ya meli, akiona, atajipa moyo tena,” alisema Longfellow. Naam. Tunaposafiri kwenye bahari adhimu ya maisha, hebu na tutoe ushuhuda wetu. Hebu tufanye jambo fulani, hata tutaacha kumbukumbu za kudumu. Kumbukumbu ambazo labda mwingine, naam, ndugu mpweke na aliyepatwa na ajali ya meli, akiona kile tulichofanya, atajipa moyo tena, ajaribu tena. Aliona ambapo mtu fulani alikuwa fukara na asiye na kitu, akajaribu na kusimama juu ya ahadi za Kristo na akawa askari wa msalaba.

<sup>121</sup> Hebu tufanye alama za miguu; alama za miguu ni umilikaji. Mungu alimwambia Yoshua, “Kila mahali nyayo za miguu yako zitakapokanyaga, nitakupa wewe.” Alama za miguu zilimaanisha umilikaji, “Endelea ukaiteke, ni yako.” Kila ahadi katika Kitabu, kila kitu Mungu alichowahi kuahidi ni chako.

<sup>122</sup> Sasa, Yeye hatafagia tu nyumba, na kusema, “Nenda ukaichukue.” Alisema, “Nimewapa Palestina,” lakini iliwabidi kupigania kila inchi ya hiyo njia. Hiyo ni kweli. Na kila inchi ya, kila wakati Mungu anapotoa ahadi, utapigania kila inchi ya hiyo njia, chukua tu upanga wa Roho na Neno na ukatilie mbali kila ibilisi na kutokuamini kutoka kwako. Kata kamba za pwani zinazokushikilia ufukoni, kisha “Twekeni mpaka kilindini mkazishushe mvue samaki.” Amina.

<sup>123</sup> Sijiitikii amina mwenyewe, *bali* amina linamaanisha, “Na iwe hivyo,” nami ninaamini hilo. Naam. Naam, bwana. Watu wengine wanaogopa *amina*, mtu fulani anaogopa *Haleluya*. *Haleluya* ni neno la Kiebrania ambalo linamaanisha, “Mungu wetu asifiwe.” Amina. Yeye anastahili sifa zote.

124 Sasa, Yohana alisema, “Nina hakika Huyu alikuwa ni Yehova.”

125 Mwajua, na Petro a—asingeweza kuketi tu pale zaidi, kwa hiyo i—ilimbidi kutoa ushuhuda wake, vema, akasema sasa, “Mumu humu kwenye bahari ii hii, ndugu, nataka kuingiza ushuhuda wangu.” Hebu tumsikilize kwa dakika chache, akishuhudia:

126 Petro alisema, “Nitawaambia kilichotukia. Nilipokuwa mvulana mdogo, Mama na Baba walikuwa wakisimama kule kwenye ufuko huo, kule chini mahali mashua zetu zilikokuwa. Baba yangu alikuwa m—mtu mashuhuri, alikuwa Mfarisayo pale kanisani, na—naye alikuwa mwaminio hodari sana. Na jinsi tulivyokuwa tukipiga magoti pale wakati hatukuwa na mkate, nasi tungemwomba Mungu atupe samaki wengi, kamwe hakutupungukia, tungeenda kuwavua samaki na kurudi ndani. Baba aliniambia nimwamini Mungu, kuamini kila Neno ambalo Mungu alisema, kila ahadi ni ya kweli, kwa hiyo daima nimeamini hilo ndugu.

127 “Ndipo basi Baba akaniambia siku moja wakati alipokuwa anazeeka na nywele zake zimeingia mvi, alikuwa akitetemeka, kwa hiyo akaniketisha u—upande wa mbele ya mashua siku moja baada ya kuvua samaki wengi, naye akasema, ‘Simoni, umeona kile Yehova ametupa leo? Mwanangu, kamwe usimsahau.’

“Loo,” anasema, “ninaweza kukumbuka maskini ushuhuda wa Baba.”

128 Wengi wenu ninyi watu mnaweza kukumbuka kitu kama hicho, jinsi maskini baba na mama yako walivyokuwa wakikuketisha chini na kuzungumza nawe habari za Mungu na kuomba pamoja nawe. Mungu, tupe watu zaidi kama hao ndipo tutakuwa na Marekani halisi, tuwaweke chini na kuzungumza nao, na kuwaambia habari za Mungu.

129 Akasema, “Siku moja, wakati akinikalisha chini, alisema, ‘Simoni, sikuzote niliomba ya kwamba ningemwona Masihi akija.’ Lakini kasema, ‘Ninazeeka sasa, nadhani sitamwona. Baba zangu wamemtazamia, nasi tumemtazamia tangu zamani za kale, tulipofanyika taifa na kumjua, tumemtazamia kuja. Lakini nadhani sitamwona, Simoni, lakini labda wewe utamwona katika kizazi chako. Simoni, kabla tu Yeye hajaja kutakuwa na mkutano mkubwa wa kila kitu, tunajua, lakini,’ kasema, ‘Simoni, kamwe usidanganyike.

130 “Sasa, ajapo Masihi, ninawatakeni mkumbuke hili: Sisi Waebrania, Naye ni Mungu wa Waebrania, na sisi Waebrania tunafundishwa ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atakuwa ni Nabii, kwa kuwa Musa alisema, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Mtiwa mafuta, Nabii, aliye kama mimi.” Na sasa, Simoni, atakapokuja, huenda kukawa na watu watakaoinuka na kufanya mambo makuu, bali wewe kumbuka

jambo hili moja, huenda kukawa na waelimishaji mashuhuri watakaoinuka, huenda kukawa na wasomi mashuhuri, huenda kukawa na madhehebu makubwa ya kanisa, huenda kukawa na mambo makuu, lakini, Simoni, Simoni, mvulana wangu. . .’

<sup>131</sup> “Nami ninaweza kumwona,” akasema, “akaweka mkono wake juu ya kichwa changu, na kusema, ‘Simoni. . . Ee Mungu, jalia mvulana wangu asidanganyike! Lakini, Simoni, kumbuka, Maandiko ndiyo yanayosema ya kwamba Yeye atakuwa ni Nabii, usisahau hilo.”

Ninaweza kumsikia akisema, “Ninaweza tu kuwazia jinsi baba yangu mzee alivyoniabariki pale. Naye akasema, ‘Simoni, utajua hilo.”

Naye akasema, “Ndugu, siku moja Andrea alinijia naye Andrea akasema, ‘Aisee, unajua nini? Tumemwona Masihi!’

“Loo, sasa, endelea.”

“Njoni, mnapaswa kuona kile alichofanya asubuhi ya leo. Njoo huku juu.”

<sup>132</sup> “Vema, nilimfuata. Na mara niliposimama Mbele za huyu Yesu, mnajua kilichotukia? Mara tu nilipoenda Mbele Zake, aliniangalia moja kwa moja usoni na kusema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’

<sup>133</sup> “Si kwamba tu alinijua, bali alimjua maskini huyo baba yangu, kwa hiyo hilo lilitosha kwangu, Yeye alikuwa ni Masihi.” Ninaweza kumwona akiinua tu mikono yake juu na kumsifu Mungu.

<sup>134</sup> Filipo akasema, “Unajua, Ndugu Nathanaeli, ni sawa?”

“Naam.”

<sup>135</sup> “Simoni, ulipokuja huko siku hiyo, na hilo likatosha kwangu, pia, niliposimama pale na nikawasikia hao Wayahudi huko nje, watu wetu, wakisema, ‘Mtu huyo ni mpiga ramli, yeye ni Beelzebuli, yeye ni ibilisi, hivyo ndivyo anavyofanya,’ lakini kwangu mimi, lilitatuliwa, Huyu alikuwa ni Masihi, nilijua hivyo. Sasa, haikumbidi Yeye kunifanyia lolote, wala kuniambia lolote, nilimwona akifanya hivyo kwa ajili ya wengine, kwa hiyo nikaamini hilo.

<sup>136</sup> “Na kwa hiyo, mimi na Nathanaeli tulikuwa marafiki wakubwa kwa miaka mingi sana, tulienda kanisani pamoja tangu utotoni. Ndipo nikakimbia kuzunguka mlima na kumwona chini ya mti, akiomba, ndipo nilipomwambia ‘Njoo umwone Yule niliyemwona, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu,’ unakumbuka, Nathanaeli, uliyoniambia?”

“Naam, nilisema hivi: ‘Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?’”

“Haya basi waambie hawa ndugu, basi, nilikwambia nini?”

“Mbona, ulisema, ‘Njoo uone.’” Vema, hilo ni jambo zuri.

“Una furaha ulikuja?”

<sup>137</sup> “Kamwe sitakusahau Filipo, kamwe sitakusahau. Nilipokuja huko Filipo aliendelea kuniambia...” Alijitokeza na ushuhuda jinsi...mbele ya Filipo, na kusema, “Filipo aliendelea kuniambia ya kwamba Mtu huyu alikuwa amesema hayo, Simoni hapa, ambaye nilijua hakuwa na elimu yoyote, na kumwambia ya kwamba jina lake lilikuwa ni Simoni, na kumpa jina lingine la *Petro*, na kusema ya kwamba jina la baba yake lilikuwa ni Yona. Nami niliwajua wote wawili Simoni na Yona, nilinunua samaki kutoka kwa wote wawili, kwa hiyo nilijua ya kwamba ndivyo ilivyo kuwa.

<sup>138</sup> “Kwa hiyo nikasema, ‘Ninaenda mkutanoni, nami nitamtazama tu Jamaa huyu nione kama huyo ndiye Masihi.’ Ninajua ya kwamba Masihi alipokuwa akija, hakika Yeye alikuwa awe ni Nabii.

<sup>139</sup> “Kwa hiyo basi, nilipomwendea, mnajua kilichotukia ndugu? Mara nilipoenda Mbele Zake, Yeye alisema, ‘Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake.’

“Nami nikasema, ‘Rabi,’ *kasisi, mwalimu*, mwajua, “ulipata kuniona lini Wewe?”

“Akasema, ‘Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.’”

Kasema, “‘Hilo lilitosha kwangu.’”

<sup>140</sup> Filipo akasema, “Sasa, ngojeni kidogo tu, ndugu. Mnakumbuka wakati ule tulipokuwa huko chini Yeriko?”

“Naam.”

“Unamkumbuka yule jamaa mdogo, Zakayo?”

“Loo,” hao ndugu walisema, “kamwe hatutasahau hilo.”

<sup>141</sup> Walikuwa na wakati mzuri huko nje wakishuhudia, giza likiingia tu, mwajua, labda muda mrefu yapata wakati huu. Nao, na kusema... Loo, kuwa tu na wakati mzuri sana.

Kwa hiyo akasema, “Unakumbuka tulipokuwa kule chini, yule jamaa mdogo Zakayo? Mnakumbuka wakati alipotoa ushahidi kule kwenye chakula cha jioni siku hiyo?”

“Naam, naam, ninaikumbuka.”

“Unamkumbuka Bartimayo?”

“Naam, nakumbuka.”

<sup>142</sup> “Sasa tunakumbuka ya kwamba Zakayo alikuwa na mke, na jina lake lilikuwa Rebeka, naye alikuwa mwaminio mzuri wa Bwana Yesu. Kwa hiyo, alikuwa ameomba kwamba mumewe, ambaye alikuwa... Mojawapo ya nguzo kuu kanisani ilikuwa ni Rabi Lavinski.” Natumaini hakuna mtu hapa mwenye jina hilo, lakini hilo ni jina tu la kubuni ninalotoa tu kwa ajili ya hadithi yangu.

<sup>143</sup> “Alisema kwamba yeye alikuwa ndiye nguzo kuu katika moja ya makanisa, kwa hiyo Rabi Lavinski akamwambia, kasema, ‘Sasa, ngoja kidogo, usiamini upuuzi huo. Huyu mwanamke wenu amefadhaika kidogo, jamaa huyo si nabii, hatujawa na manabii kwa mamia na mamia na mamia ya miaka. Usiamini hilo, hilo ni lundo la ushupavu wa dini, kama yule mtu mkali anayejaribu kumzamisha kila mtu kule chini Yordani, Yohana; Herode akamkata kichwa. Jamaa huyu atafikia ki—kikomo chake moja ya siku hizi. Usiamini upuuzi huo.’

<sup>144</sup> “Nanyi mnakumbuka Zakayo alifikiri rabi alikuwa sahihi, maana alifundishwa kuamini ya kwamba rabi wake alikuwa sahihi kabisa. Sasa, tunaona ya kwamba, mwajua, lakini Rebeka alituomba sote tumwombee Zakayo. Nasi sote tungekuwa tukiomba, kwa sababu tunajua Bwana wetu alikuwa akishuka kwenda kule kufanya mkutano siku moja.

<sup>145</sup> “Kwa hiyo tukashuka kwenda kule kufanya mkutano asubuhi hiyo, naye Rebeka akatwambia ya kwamba Zakayo alihangaika sana. Naye alikuwa akimwombea usiku kucha, ili aweze kumwona Yesu kesho yake, kwa sababu alijua kungekuwa na wengine watakaomwunga mkono na wengine watakaompinga.” Hivyo ndivyo ilivyo katika kila mkutano.

“Kwa hiyo, kwa hiyo, alisema alikuwa, aende kule chini, kwa hiyo asubuhi na mapema akaamka na kujiandaa na kuvaa vazi lake lililo bora zaidi, kisha akatoka nje.

“Akasema, ‘Zakayo, kwani unaenda wapi?’

“‘Ninatoka tu nipate upepo baridi kidogo asubuhi ya leo, ninajisikia kusongwa kidogo, sikulala vizuri jana usiku.’

“Akageuka, akasema, ‘Asante, Bwana, asante. Unahusika na yeye, unahusika na yeye.’”

<sup>146</sup> Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya, ninyi wanawake waombeeni waume zenu namna hiyo, mnaona, kwa hiyo, nanyi waume umwombee mke wako, pia, na sasa, ninyi watoto waombeeni wazazi wenu wakaidi, pia, mnapofanya hivyo, mnaona.

<sup>147</sup> Kwa hiyo basi, wao... “Alishuka akaenda mtaani, akatwambia, kisha akasimama pale, moja kwa moja langoni, maana alijua Yesu alikuwa akishuka kutoka Yeriko. Kwa hiyo akasema... wakati yeye—yeye, aliposhuka, uh, akishuka kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko, kutoka mlimani.

<sup>148</sup> “Kwa hiyo basi, tulipoenda langoni, alikuwa ni maskini jamaa mdogo, mwajua, kwa hiyo asingeweza, a—asingeweza kuwaangalia watu, alikuwa ni jamaa mdogo. Kwa hiyo akakimbia kwenye barabara nyingine inayoitwa Barabara ya Haleluya, moja kwa moja mahali Barabara ya Utukufu inapoingilia, na kulikuwa na...” Hapo ndipo daima unamwona Yesu, kwenye Barabara ya Haleluya penye Barabara ya Utukufu,

kwa hiyo alijua angepitia njia hiyo, pia, hivyo ndivyo mimi, yeyote wetu anavyompata, kwenye barabara hiyo.

<sup>149</sup> “Kwa hiyo akaangalia kule chini na kusema, ‘Unajua nini? Atakuwa hapa, lakini unajua umati uo huo huambatana Naye popote aendapo.’” Hiyo ni kweli, hiyo ni kweli, huenda pamoja Naye popote aendapo. “‘Halafu basi, watakuwa hapa, kwa hiyo nitakuwa mdogo tu wakati huo kama nilivyo sasa, kwa hiyo sitakuwa bora hapa, kuliko vile ningekuwa nikisimama langoni.’” Maana walikuwa wamening’inia nyuani kule chini, na juu ya ukuta, wakimngojea. “‘Kwa hiyo unajua nini? Ninaamini nitapanda juu ya mti huu hapa, ndipo basi ninaweza kumwona.’

<sup>150</sup> “Kwa hiyo anaenda kule na kuchukua ndoo ya takataka na kuibeba na kuiweka chini, anaparamia juu ya mti, mwajua, anapanda kule juu. Ndipo akaona ambapo matawi mawili yanapokutana ili aweze kujiandalia kiti kizuri, akaketi chini,” (Hapo ni mahali pazuri pa kuketi na kuwazia, ndugu, ambapo njia mbili zinakutana, yako na ya Mungu.) “yatafakari, umeketi pale kwenye tawi.

<sup>151</sup> “Naye akasema ya kwamba aliketi chini pale, ndipo akaanza kusema, ‘Sasa, nitajuaje wakati Yeye atakapokuja? Atakapokuja huku, atageukia hapo, kutoka kwenye Barabara ya Utukufu pale, ashuke kwenye Barabara Kuu ya Haleluya, na atakapogeukia hapa, nitamchungulia vizuri, maana atakuwa katikati ya barabara atakapopitia hapa, na baadhi ya hao watu wakimsukumia kila mtu mbali Naye, nitamwona vizuri. Mwajua, Rebeka aliniambia ya kwamba Huyu alikuwa, Mtu huyo alikuwa ni Nabii, ya kwamba angeweza tu... Yeye alikuwa ni Masihi kweli. Sasa, kama Yeye ni nabii, Yeye ni Masihi, ila Lavinski aliniambia ya kwamba Yeye hakuwa nabii, Yeye alikuwa tu ni mtu wa kujifanya mwaminio, Yeye ni nabii tu wa kujifanya mwaminio.

<sup>152</sup> “‘Halafu basi asubuhi ya leo pia, kuhani mmoja alishuka kutoka huko Yeriko, alikuwa kiongozi wa shirika la wahudumu, naye alishuka kuja hapa kuhakikisha hawatafanya ibada ya uponyaji hapa, kwa hiyo akamfukuza mzee huyo kipofo kutoka langoni huko nje akiomba, maskini Bartimayo, mnaona. Kwa hiyo yuko humu ndani kuhakikisha ya kwamba hawana ibada ya uponyaji hapa miongoni mwa watu hawa. Kwa hiyo nadhani ni kundi tu la ulokole, kwa vyovyote vile, kwa hiyo nitaketi hapa.

<sup>153</sup> “‘Sasa, ngoja kidogo, vipi kama akipiga kona hiyo? Angeniona nimeketi hapa juu ya mti huu. Niko juu sana, lakini mwajua, kama nitashusha baadhi ya majani haya makubwa chini namna hii, na kwa namna fulani nijifiche, hataniona kamwe. Nami nitamwangelia atakapopita, ndipo nitarudi na kumwambia Rebeka yote kumhusu, nitawaambia ya kwamba Jamaa huyo ni bure. Ninajua tu sitamwamini, la, bwana. Kwa hiyo, Yeye hataniona; nami nimeketi hapa juu nimejaa takataka

hizi mwilini, kwa vyovyote vile, kutoka kwenye ile ndoo ya takataka.”

<sup>154</sup> Unajua, wakati unapokuwa, unapowazia kukutana na Yesu, Yeye atakufanya ufanye baadhi ya mambo ya kipumbavu sana, Yeye ata—Yeye ataharibu tu sifa zako zote. Unafikiri hutapiga nduru, na kulia, na *kupiga makelele*, bali utafanya hivyo kama unataka kumwona Yeye, uta—utafanya tu lolote upate kumwona. Hiyo ni kweli.

<sup>155</sup> “Kwa hiyo huyo hapo ameketi, kasema, ‘Vipi kama naniii wangu, baadhi ya washindani wangu wakipita, na kuniona nimeketi hapa juu? Kwa hiyo nitajificha vizuri sana, asiye mtu akaniona.’ Kwa hiyo akavuta majani yote kando yake na kujifunika matawi mtu yeyote asiye akamwona.” Kisha akaacha jani moja dogo kama mlango, loo, labda kitu kama *hiki*, basi akaliacha hapa, naye angeweza kulishusha, aangalie na kuona wakati alipokuwa akija, halafu aliinue juu tena.

<sup>156</sup> “Akasema, ‘Ni—nitamwona, na ndipo nitajua ninapomwangalia, ninaweza kujua Yeye ni laghai. Yeye si kitu zaidi ya mtu mwingine yeyote, hivyo tu. Nami nitamwambia Rebeka nitakaporudi, “Jiepushe na laghai kama Huyu,” hivyo tu.’

<sup>157</sup> “Baada ya kitambo kidogo ikatokea kelele.” Jambo la ajabu, kila mahali alipo Yesu kuna kelele nyingi sana, sijui ni kwa nini, bali ni—ni ishara ya kwamba kuna Uzima hapo. Mnajua wakati kuhani alipoingia mahali pa juu... mahali patakatifu alikuwa na komamanga na kengele, ilimbidi kupiga kelele kusudi watu waweze kuelewa alikuwa angali hai. Nafikiri baadhi ya makanisa haya yanahitaji kuzikwa, yamekufa muda mrefu uliopita, husikii kelele hata kidogo. Ni kama nyumba ya maiti badala ya ma—mahali pachangamfu, mahali panapowaka moto kwa ajili ya Mungu.

<sup>158</sup> “Ndipo akasema, ‘Nitaketi hapa nyuma sasa nipate kumwangalia.’ Na yapata tu wakati huo, akasikia kelele ikija, akaangalia pembeni, akasema, ‘Uh-huh, Yeye atakuwa akija.’

<sup>159</sup> “Alimwona mvuvi huyu mkubwa mno akitembea pale, akiwasukumia upande mmoja, ‘Samahani, jamani, Ndugu ye—ye—yetu amechoka sana, sana, uh, Bwana wetu amechoka sana, sana, amekuwa nje usiku kucha. Anaenda Zake hapa chini kuwaona baadhi ya marafiki Wake. Samahani, kamwe hatutakuwa na wakati,’ vizuri sana.

“Huku mitume wakija, ‘Samahani, hatuna budi kufanya hivi,’ kiungwana sana.

<sup>160</sup> “Na—na kwa hiyo, nadhani lazima Zakayo alisema, aliwaambia, ‘Mnajua, kidogo ni jambo la kigeni, lakini hao watu ni waungwana.’ Mnajua, mtu yeyote anayemtumikia

Bwana Yesu ni mwungwana, mnaona, kwa hiyo basi, kwa heshima.

<sup>161</sup> “Kwa hiyo basi, baada ya kitambo kidogo, akakata kona, akasema, ‘Unajua nini? Jamaa huyo anaonekana tofauti kidogo. Mi—mimi ninaninii tu, Yeye...’” Unajua, hakuna mtu anayeweza kumtazama Yesu na abaki vile vile, utakuwa mkosoaji mbaya zaidi, ama mtu bora zaidi, hivyo tu, unaona.

<sup>162</sup> “Kwa hiyo akasema, akamtazama, alikuwa na jani hili, kasema, ‘Sasa, Yeye kamwe hataniona, kamwe hataniona. Sasa, Rebeka alisema Yeye alikuwa ni Nabii. Kwa hiyo, Yeye kamwe hataniona.’

<sup>163</sup> “Naye alimtazama tu mpaka akafika papo hapo chini namna *hiyo*. Yesu akaja ameinamisha kichwa Chake, akitembea kama alivyofanya kwa kawaida katika hatua Yake ya kawaida, akafika papo hapo chini ya huo mti, akaangalia juu, na kusema, ‘Zakayo, shuka chini, ninaenda nyumbani pamoja nawe kwa chakula cha kutwa.’

“Mnakumbuka aliyosema Zakayo? Hilo liliondoa ugumu wote ndani yake. Naam, bwana. Maana alijua Yeye alikuwa ni Nabii.

<sup>164</sup> “Nanyi mnakumbuka?” Filipo akasema, “Mnakumbuka ndugu, tulipotoka nje ya lango, nasi, ushuhuda huo mwingine tulio nao nje ya lango? Hapo mwajua, walisikia kelele ikija, wakati Bartimayo alipotushuhudia, akasema alikuwa ameketi pale akiota hadithi za Biblia ambazo mama yake alimwambia alipokuwa mvulana mdogo, kama tu vile Yohana alivyokuwa akishuhudia, na kusema jinsi mama alivyomwambia jinsi Yehova alivyokuwa mkuu, na jinsi ambavyo papo hapo kwenye barabara iyo hiyo, hayo mango mahali alipokuwa ameketi, kwamba Elisha na Eliya walikuja, wameshikana mikono moja kwa moja chini ya barabara hiyo, wakishuka kwenda kuvuka Yordani.” Amina!

<sup>165</sup> “Loo, laiti ningaliishi katika siku hiyo, ningewakimbilia na kusema, “Enyi manabii wa Mungu, nirehemuni na mniombee,” naye Bwana angeyafungua macho yangu. Lakini, ole, rabi ananiambia, kuhani, ya kwamba siku za miujiza zimepita.’

<sup>166</sup> “‘Nami nakumbuka basi kwamba Yoshua alivuka ule mto,’ kasema—kasema Bartimayo, ‘alivuka ule mto si yadi mia tano kutoka mahali ninapoketi, na yule Yoshua mashuhuri, Mungu, akayarudisha maji nyuma katika mwezi wa Aprili wakati yalipokuwa karibu maili moja hapa bondeni, na kuyarudisha nyuma, na kusimama kimya, nayo hayo maji yakashikilia mahali pao, huko juu mi—mi—milimani. Maji ya theluji yalishikilia mahali pake wakati Waisraeli milioni mbili na nusu walipovuka na kupiga kambi.’” Loo, jamani!

<sup>167</sup> “‘Laiti ningalikuwa tu nimeketi hapa wakati huo! Nami nimeketi kwenye miamba, papa hapa asubuhi ya leo,’ akasema,

‘iliyoanguka wakati Yoshua, wao walipiga tarumbeta, ndipo Mungu akaziangusha hizo kuta, nayo nyumba ya Rahabu kahaba ikasimama, kwa sababu aliamini.’

168 “Ndipo basi Yoshua, siku moja wakati alipokuwa huko nje, yule mtu mashuhuri, akitembea huku na huku, akiangalia kote makondeni, akiona jinsi ninii kuu... akiichunguza hali hiyo, alimwona Mtu amesimama amechomoa upanga Wake, ndipo Yoshua akauchomoa upanga wake, akaenda kumkabili, akasema, “Je, Wewe uko pamoja nasi, uko upande wa adui zetu?”

“Akasema, “Mimi ni Amiri wa jeshi la Bwana.”

“Yoshua akatupa kofia yake ya chuma, na kuitupa chini ngao yake, akaangusha upanga wake, akaanguka magotini mwake.

169 “Loo,’ akasema Bartimayo kipofu, ‘laiti ningalikuwa pale wakati huo, ningemkimbilia huyo Kapteni Mkuu na kusema, “Kapteni Mkuu wa jeshi la Bwana, unirehemu, kipofu.” Nangepata kuona.” Hakujua kwamba umbali wa yadi mia moja kutoka kwake Kapteni yule yule alikuwa anakuja, akielekea langoni.

170 Loo, laiti Kanisa hili lingeweza kutambua, usiku wa leo, Kapteni yuyo huyo, “Sitakuacha kamwe wala sitakupungukia. Nitakuwa pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari. Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona,” Kanisa lililoteuliwa, “mtaniona Mimi, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi. Kazi nizifanyazo, ninyi pia mtakuwa mkizifanya, hata mwisho wa ukamilifu wa dahari, ulimwengu,” utaratibu wa ulimwengu.

171 Sasa angalieni, naye akasema, “Mnakumbuka yale Bartimayo kipofu aliyoshuhudia? Alipopitia pale, alisema watu wote walikuwa wakipiga makelele na wengine wakipiga mayowe, ‘Mwondoeni huyo laghai!’ Nao walikuwa wakimtupia mayai yaliyoza na nyanya zilizoza. Sasa, alisema angeweza kumsikia kasisi huyo akisema, ‘Aisee, wewe uliyewafufua wafu! Unaniambia walimfufua mtu aliyekufa jina lake Lazaro, tuna makaburi yaliyojaa hao hapa juu, njoo ukawafufue baadhi yao, tutakuamini.”

172 Mnaona, ibilisi yuyo huyo wa kale? Yuyo huyo alimjia, akasema, “Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, fanya jambo fulani hapa mbele zangu. Hivi wewe...? Kuna makanisa fulani yanayotaka kujua hilo.”

“Tuna kipofu ambaye huketi pembeni, nendeni mkamfungue macho, enyi waponyaji wa Kiungu.”

“Ninaye maskini Ndugu *Nanii* anayeza penseli hapa chini, njoo umponye.”

Kumbuka tu huyo ni ibilisi yule yule aliyesema, “Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yageuke kuwa mkate.”

<sup>173</sup> Siku moja walimfunga tambara kichwani namna *hiyo* na kumzungushia, kisha wakachukua fimbo na kumpiga kichwani katika nyua za Pilato, na kusema, “Kama wewe ni nabii na unaweza kujua siri za mioyo, kama wewe ni Masihi, na kama wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga.” Yeye hakufungua kinywa Chake na kusema Neno. Yeye hawafanyii watu vitimbi, Mungu hawafanyii watu vitimbi, Yeye husema tu, “Sifanyi neno mpaka Baba anionyeshe. Lile nimwonalo Baba analitenda, ndilo nitendalo pia,” Yohana Mtakatifu 5:19.

<sup>174</sup> “Nanyi mnakumbuka, Bartimayo alitwambia,” kasema Filipo... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “...?...kwamba tulimsikia Zakayo akishuhudia kwenye karamu, muda mfupi uliopita, juu ya yale Yeye aliyomwambia, naye alijua alikuwa kwenye mti juu Yake, pia alijua jina lake lilikuwa Zakayo, kisha akamwita atoke mtini akaenda pamoja naye nyumbani kwa chakula cha kutwa. Zakayo anauwasha moto mji kwake kwa hilo. Kwani huyajui Maandiko, bwana?”

“Loo, ninakumbuka nilipokuwa mvulana mdogo mama yangu alikuwa akinisomea Magombo. Lakini ni Nani huyu unayenena habari zake? Yesu Nani?”

<sup>175</sup> “Yesu wa Nazareti. Yeye ni Nabii wa Galilaya, wanavyomwita, lakini kwa kweli, Yeye ndiye Masihi. Yeye hufanya ishara ya Masihi, Yeye ni Nabii. Vema, unajua Ma—Masihi atakuwa ni Nabii.”

“Hakika. Vema, ulimjuaje?”

“Mimi ni mtumishi Wake.”

<sup>176</sup> Mnajua, watumishi wote wa Yesu, watumishi wanawake ni wema, na watumishi wanaume ni wema, kuwafikiria wagonjwa na wanaoteseka. Mkutano unapokuja mjini, wanamwalika kila mtu na kujaribu kuwafanya watoke. Wao, mwajua, wa—wanajaribu kufanya jambo fulani, wanawapenda watu, wanafunzi wa kweli wa Yesu. Mnaamini hilo sivyo? Natumai hili linakolea.

<sup>177</sup> “Kwa hiyo basi muda si muda mwajua, alimwambia, kasema, ‘Vema, hakika, naam, mi—mi—mimi, mnaona, mimi ni mwanafunzi Wake. Na kwa hiyo, mimi na Dada Rebeka tulikuwa tukiomba, hu—huyo ni Zakayo...’ Kasema, ‘Unamjua Zakayo?’

“Loo, naam, amenipa sarafu hapo awali. Vema, huyo... Na Yeye yuko wapi?”

“Loo, anateremka huko mbali barabarani sasa.”

“Anafanya, ‘Loo, loo!’ Akatupa chini koti lake, na kupiga makelele, ‘Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu! Unirehemu!”

“Baadhi yao wakasema, ‘Nyamaza, keti chini, acha kupiga kelele nyingi.’ Mnaona?”

“Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.”

<sup>178</sup> Sasa, tukinena kibinadamu, Yeye asingeweza kumsikia. Yeye, kama ukiona ambapo hayo malango alipokuwa ameketi na mahali Yesu alipokuwa wakati huo mwujiza ulipofanywa ni yapata yadi mia tatu na hamsini. Mnaona? Huku umati huo wote ukifuata pale na kupaza sauti, “Salamu, salamu kwa—kwa Mfalme wa Wayahudi!” Au neno la fedheha. Wengine wakapaza sauti, “Hosana, kwa Nabii!” Na kusema kila kitu, Yeye kamwe hakisikia. Lakini akasema. . .

<sup>179</sup> Ninaweza tu kuwazia nikimwona Bartimayo akipiga magoti na kusema, “Ee Yehova, nilikuwa nikikuwazia Wewe.” Hapo ndipo Yeye anapokuja, ni wakati unapomwazia. Acha kuwazia mambo ya ulimwengu, na ni nani atakayekuwa bingwa wa sinema, au hata Rais ajaye, na uwazie kwamba Kristo ajaye ni Nani, ndipo utambariki.

<sup>180</sup> “Loo, loo, Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, Bwana Yehova Mungu, kama Huyo ni Mwanao, kama Yeye ni Mwana wa Daudi, kama huyo ndiye yule Nabii, mbona, Wewe unaweza kuzungumza Naye. Ee unirehemu, unirehemu.”

<sup>181</sup> Naye Yesu, akiwa na dhambi za ulimwengu mabegani Mwake, alikuwa akielekea moja kwa moja Yerusalemu kusulubiwa. Ee Mungu, dhambi ya kila mwanamume na kila mwanamke aliyepata kuishi, ama angepata kuishi iliwekwa juu Yake, mzigo wa kama tungeokolewa, mzigo wa mkutano huu usiku wa leo, ulikuwa mabegani Mwake, lakini imani ya ombaomba mmoja kipofu ilimsimamisha, Biblia ilisema Yeye alisimama. Laiti ningalikuwa na majuma machache tu ya kukaa hapa, ningetaka kuhubiri juu ya *Ndipo Basi Yeye Akasimama, Yesu Akasimama Kimya*.

<sup>182</sup> Imani moja ya ombaomba ilimsimamisha, Naye akasimama kimya. Ni kitu gani kilichosababisha hilo? Imani Yake ilimgusa, kama tu yule mwanamke aliyegusa vazi Lake, “Ni nani aliyenigusa?”

<sup>183</sup> “Ndipo akageuka, akasema, ‘Mleteni hapa. Mnataka niwafanyie nini?’ Imani yake ilikuwa imengusa.” Kama tu vile unavyomgusa Yeye hapa usiku, unaona, jambo lile lile.

“Nanyi mnakumbuka ndugu kilichotukia? Alipata kuona. Sasa, mnakumbuka hilo?”

“Naam, ndugu,” hao ndugu wakamwambia Filipino, “Nakumbuka hilo.”

<sup>184</sup> Hapana shaka ilikuwa ni Andrea, kasema, “Mnakumbuka siku ile wakati sote tulipokuja kisimani, tulipoenda Samaria kununua chakula? Tulifika kisimani, ndipo tukamwona mwanamke huyu Msamaria.”

<sup>185</sup> Tunajua kamwe hakufanya hivyo mbele ya Mmataifa, alisema ingekuwa kwa ajili ya wakati mwingine, Yeye angefanya hivyo Mwenyewe katika wakati mwingine kwa Mataifa, bali hawakumwamini. Yeye huja tu kwa wale, na kujionyesha Mwenyewe kwa wale wanaomngojea, hivyo tu. Hiyo ni kweli. Ndio pekee anaowafunulia, ambao Yeye hujifunulia Mwenyewe.

Sasa, angalieni, tunapofunga katika dakika chache tu.

<sup>186</sup> Andrea akasema, “Sisi sote tulitoka kisiri kununua vyakula, ndipo tuliporudi, mnakumbuka tulimwona mwanamke akija, akitembea polepole kuelekea kisimani, nasi tulijua alikuwa ametiwa alama kama mwanamke mwenye sifa mbaya?”

“Naam, ninaikumbuka,” wote.

<sup>187</sup> “Nasi tukaingia kisiri nyuma ya mahali pale na kusikia yaliyosemwa, basi alipozungumza naye kidogo, ndipo Yeye akasema, ‘Nenda, kamwite mumeo.’

<sup>188</sup> “Naye akasema, ‘Sina.’ Mnakumbuka jinsi mioyo yetu ilivyohuzunika? Nasi tukasema, ‘Loo, jamani, jamani! Huo hapo wakati mmoja alipokosea, huyu mwanamke analikana.’”

<sup>189</sup> Loo, hakika, huenda wakakana, Sara alilikana, pia, alisema, “Kamwe sikusema.”

<sup>190</sup> Lakini Malaika akasema, “Naam, lakini ulisema hivyo.” Nami ninataka kuwapa chembe ndogo ya neema hapa, Mungu angalimwua papo hapo, bali asingeweza, yeye alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu. Katika dhambi zetu, tungeuawa na Mungu, kama hatukuwa sehemu ya Kristo, Yeye... inalishikilia. Mnaona? Sisi ni—ni Bibi-arusi, inaishikilia. Naam, bwana. Hilo ndilo Balaamu alishindwa kuona kule chini, kama tulivyokuwa tukizungumza hivi majuzi usiku. Mnaona?

<sup>191</sup> “Naam, naam, tunakumbuka.”

<sup>192</sup> “Lakini aliangalia pande zote, akasema, ‘Umesema kweli. Umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye wako.’ Hivi...? Naye akakimbia mjini. Nanyi mnakumbuka kile mwanamke huyo alichomwambia huyo, Yeye?

“Alisema, ‘Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii.’

<sup>193</sup> “Sasa, ni tofauti jinsi gani kati ya ushuhuda wake na ule Mafarisayo walikuwa ndio kwanza watoe! Kasema Yeye alikuwa ibilisi. Basi aliwaambia kuita kazi ya Mungu ibilisi kungewatenganisha, daima, na Mungu. Mnaona? Na kwa hiyo, Yeye alisema, ‘Vema, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe.’”

<sup>194</sup> Sasa, yeye alisema, “Uliona, alikimbia mjini na kusema, ‘Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Ndipo sote tulishawishika na kujua ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi.”

195 Walipokuwa wakishuhudia, hivi si ungetaka kuwa umeketi kwenye meli hiyo ukiwasikiliza? Loo, jamani! Lakini tunaweza kuwasikiliza, pia, mnaona, tunao tu ushuhuda wao, kile—kile wangesema. Kwa hiyo mkutano huo wa ushuhuda ukiendelea, na wote, walikuwa wamekuwa na wakati mzuri sana siku hiyo, mwajua, mkutano mkubwa. Ilikuwa ina- . . .

196 Mnajua nini? Bila shaka Shetani alichungulia kwenye milki za kuzimu, na kuwaona huko nje majini wakifanya mkutano wa ushuhuda bila Uwepo Wake. Nao walipofanya hivyo, mwajua, walikuwa wameondoka bila Yeye. Nao. . .

197 Shetani akasema, “Hii hapa nafasi yangu, wameondoka bila Yeye.” Kweli. Hilo ndilo jambo lile lile ambalo limetukia sasa, Shetani ameliona kanisa likiendea shamrashamra kubwa za ujenzi, na shamrashamra kubwa mamboleo, nalo limemwacha Yesu. Hiyo ni kweli.

198 Yote tunayowazia ni kwamba ni wangapi tunaoweza kuwaingiza kwenye dhehebu letu; ni kanisa kubwa jinsi gani tunaoweza kujenga kuliko hayo mengine. Hilo halina uhusiano wowote nalo. Tunachohitaji ni kurudi kwenye Biblia.

199 Angalieni jinsi watu wetu walivyo, ambapo kanisa ni dhaifu, na imani ni dhaifu, nao hao watu ni ninii tu, huwezi kuwatofautisha na mtu mwingine yeyote, na ushuhuda wao ni dhaifu. Na—nao wanakaa nyumbani Jumatano usiku kutazama namna fulani ya kipindi cha televisheni badala ya kwenda kanisani. Na—nao wanafanya mizaha, na wao pia, wengi wao walianza kufanya mambo yasiyofaa.

200 Nao wanawake wameanza kuvaa kama mambo ya ulimwengu, na kukata nywele zao, na kujipaka rangi na vikorokoro kila mahali, na—na kadhalika, nao wanaume wakivuta sigara, biri, na vitu kama hivyo, na kuishi kanisani, wakinywa pombe kidogo pamoja na bosi wao, “kuwa na maskini burudani safi,” wakitoka nje na mke wa mtu mwingine, na mambo yote namna hiyo, kubembana na wasichana mtaani, wakigeuza shingo zao wakiwaangalia wanawake waliovalia nusu uchi. Hakika. Hiyo ni kweli. Ninajua hilo linaumiza, lakini hiyo ni kweli, ndugu. Neno la Mungu ni Mtahiri, hiyo ni “kukatilia mbali nyama ya ziada,” hiyo ndiyo kweli hasa.

201 “Kufanya maskini burudani safi, ya Kimarekani,” ambayo haiambatani na Ufalme wa Mungu, haihusiki na Ufalme wa Mungu, hata kidogo. Jina la Bwana libarikiwe! Inatupasa kujiendeleza kama watumishi wa Mungu. Inatupasa . . .

202 Hapa wakati fulani uliopita, walipokuwa na utumwa huku kusini, walikuwa wakiwachukua watumwa na kuwauza sokoni, kama tu vile ungefanya na farasi, ama chochote kile, kamwe haikuwa sahihi. Mungu—Mungu alimfanya mwanadamu, mwanadamu akawafanya watumwa. Ndipo basi wakati

wangefanya hivyo, wangekuja na kuchukua bili ya mauzo ya mtu, na kuwasafirisha na kuwauza, na kuwauza ili ku- . . .

<sup>203</sup> Siku moja kulikuwa na dalali aliyekuja kununua watumwa, akasema, “Una wangapi?”

Kasema, “Wapatao mia moja huko nje.”

<sup>204</sup> Akatoka kwenda kuwaangalia. Walikuwa na huzuni, wangekuja, Makaburu waliwaleta kutoka Afrika na kuwaweka huku chini karibu na Kuba, kisha wakawaleta huku na kuwauza Wamarekani hapa kama watumwa. Halafu basi, kamwe hawangerudi nyumbani tena, wangekufia huku. Walikuwa mbali na Baba, mbali na Mama, mbali na watoto, wametenganishwa, lilikuwa ni jambo la kuchukiza sana. Nao hawangefanya kazi, ingewabidi kuwacharaza, kuwafanya wafanye kazi, kwa sababu walikuwa na huzuni sana.

<sup>205</sup> Lakini dalali huyu akamwona huyu kijana mwanamume, ndugu, haikuwabidi kumcharaza. Alikuwa chonjo, chonjo kabisa, kifua nyuma na kichwa chake juu.

Mnunuzi huyo akasema, huyo dalali akasema, “Aisee, ninataka kumnunua mtumwa yule.”

Lakini mwenye mali akasema, “Hauzwi.”

Kasema, “Vema, kwa nini hauzwi?”

Kasema, “Maana, simwuzi.”

Akasema, “Ye—yeye ndiye boshi wa hao wengine?”

Kasema, “La, yeye ni mtumwa tu.”

Kasema, “Bila shaka unamlisha tofauti na hao wengine.”

Kasema, “La, bwana, yeye hula kwenye manchani pamoja na hao wengine, yeye ni mtumwa tu.”

Kasema, “Vema, ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana na hao wengine?”

<sup>206</sup> Mwenyewe akasema, “Nilishangaa kwa muda mrefu, pia. Lakini siku moja nikagundua kwamba baba yake, huko kwenye nchi ya uenyeji wake, ndiye mfalme wa kabila hilo, na ingawa yeye ni mgeni, mbali na nyumbani, angali anajua yeye ni mwana wa mfalme, naye anatenda kama mmoja.”

<sup>207</sup> Kama hilo lingemfanya Mnegro, akijua baba yake ni mfalme huko Afrika, kuenenda miongoni mwa watu wake kama mwana wa mfalme, linapaswa kutufanyia nini mimi na wewe ambao tumezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu? Tunapaswa kuwa maisha ya namna gani? Tunapaswa kuenenda kwa njia gani? Si kama mnyonge, na kurudi nyuma, na kurushwarushwa na kila kitu, na kuamini nusu, na mambo ya ulimwengu na kuingia mbio mbio. Tuinueni vichwa vyetu kuelekea Kalvari, na kuamini kila Neno alilosema Mungu na kila ahadi, na kuenenda kama wanaume na wanawake wa Mungu. Msivae kama hawa

Mayezebeli, na kutenda kama wao hapa. Hiyo ni kweli. Msifanye hivyo, inasikitisha.

208 Kuna mwanamke mmoja tu aliyewahi kujipaka rangi apate kukutana na Mungu, uh, kuninii, sio kukutana na Mungu kamwe, katika Biblia kuna mwanamke mmoja tu aliyewahi kutumia rangi, na huyo alikuwa ni Yezebeli, Mungu akamlisha kwa mbwa. Kwa hiyo, mnaona, kwanza kabisa yeye ni nyama tu ya mbwa, kwa hi—hiyo, machoni pa Mungu, kwa hiyo kumbuka tu, ndugu.

209 Loo, enyi wanawake, wanaume, jinyosheni! Enyi wanaume, mnawezaje kulistahimili? Ungemwachaje mke wako avute sigara, na kutoka nje mtaani na kutenda hivyo? Kuna nini? Mmeenda kombo na kanisa.

210 Enyi Wapentekoste, kwani mna shida gani? Kuna nini? Mlienda kombo kwa jengo kubwa ama hamaki za kidhehebu, na kumwacha Yesu nje.

211 Badala ya kumpata mhubiri wa mtindo wa kale ambaye angeihubiri kweli, mna maskini jamaa dondoadume aliyetokea, kupitia shule fulani, labda ni mjukuu wa Mungu anayewazia zaidi juu ya chakula kuliko anavyoifikiria Biblia, wala hatasema kweli juu Yake. Tunachohitaji ni watu watakaohubiri Injili na kuishughulikia kwa nguvu za Mungu, kusema kweli, haidhuru kama madhehebu yatamfukuza. Inaleti tofauti gani? Naam, bwana. Tunahitaji watu wa Mungu waliotiwa mafuta na Roho Mtakatifu ambao watahubiri Injili bila kujali yale mashirika na madhehebu yanasema juu yake. Haileti tofauti kwa vyovyote vile, tunamtetea Mungu. Amina!

212 Loo, jamani! Ninajisikia wa kidini. Naam, bwana. Naam, huenda mkafikiri mimi nina kichaa, labda ninacho, lakini niacheni, ninajisikia vizuri zaidi hivi kuliko nilivyojisia vinginevyo, kwa hiyo niacheni tu hivi. Na—najisikia vizuri namna hii, ni ajabu, maana uko huru, hujifungi na chochote, umefungwa tu kwenye vifungo vya upendo.

213 Usiache mtu yeyote akwambie ya kwamba uko huru katika taifa hili, huko huru. Kamwe huko huru, wewe ama ni mtumwa wa Kristo na upendo Wake, ama wa ibilisi, wewe ni mtumwa wa ibilisi na mambo yake; wewe ni mtumwa wa kitu fulani. Nina furaha kuwa mtumwa wa Kristo. Amina. Nimesulubiwa kwa mambo ya ulimwengu, hata hivyo ni hai, si mimi, bali Kristo anaishi ndani yangu. Amina na amina na amina!

214 Loo, jamani, laiti watu wangaliweza tu kuona jambo hilo! Laiti wangaliweza tu kuifungua mioyo yao na kuona kwamba ni kurudi kwenye Biblia, kumrudia Kristo, kurudi msalabani, kurudi kwenye Injili! Naam. Hivyo ndivyo ilivyo. Loo, Jina la Bwana libarikiwe!

215 Ibilisi aliona kanisa likiingia katika hamaki kubwa: “Sisi ni Assemblies. Sisi ni Church of God. Sisi ni Umoja. Sisi ni wa

Uwili,” na mambo haya mengine yote. Kwa nini hamkukaa jinsi mlivyokuwa? Kwa nini hamkukaa jinsi Mungu alivyowaandalia?

<sup>216</sup> Kosa kubwa sana ambalo Israeli waliwahi kufanya, wakati neema ilikuwa tayari imewapa nabii, ikawapa mwana-kondoo, na kuwapa uamsho mkubwa sana waliowahi kuwa nao, nao walikuwa wamesimama kwenye ufuo wa—wa Bahari ya Chumvi, wakicheza katika Roho, na kuimba katika Roho, na wakiwa na yubile, katika Kutoka 19, hawakutaka jambo hilo, walitaka theolojia ambayo wangeweza kubishania. Hiyo ni kweli. Kweli. Na nini? Walikuwa tu yapata siku nne mbali na nchi ya ahadi. Kosa lile lile ambalo baba zetu wa Kipentekoste walifanya, si muda mrefu uliopita.

<sup>217</sup> Ni kidogo vipi...? Ungaliweza kuwaambia walikuwa miaka arobaini kutoka kwenye nchi ya ahadi. Iliwabidi kwenda kuchukua kitu ambacho wangeweza kubishania. Vivyo hivyo na Pe... Mungu aliwafanyia nini? Aliwaacha nyikani kwa muda wa miaka arobaini. Walifanya nini? Walikuza mazao, na kuwalea watoto, naye Mungu akawabariki, hiyo ni kweli, nao walikuwa mashuhuri.

<sup>218</sup> Lakini siku moja Mungu alisema, “Mmekuwa kwenye mlima huu muda mrefu kutosha. Hebu tuamkeni twende kaskazini tukaichukue ile ahadi.” Hiyo ni kweli. Wakati wapiganaji wote wa kale walipokufa, alingojea mpaka wale wapiganaji wa kale wakafa, hiyo ni kweli.

<sup>219</sup> Sasa ndugu zetu wa Kipentekoste wamefanya jambo lile lile, badala ya kukaa tu. Unasema, “Vema, wanatoa ile Hoja Mpya.” Ni—ni nini Hoja Mpya? Na vipi kuhusu hiyo hata hivyo? Haiwabidi kujiundia dhehebu, na hizo hoja mpya hazikuwabidi kujiundia dhehebu kutoka kwake, kufanya kundi dogo na kuwatenganisha ndugu, na kuzozana, na kupigiana makelele.

<sup>220</sup> Kama halikuwa la Mungu, halitafaa chochote, kwa vyovyote vile. Na kama ni la Mungu, ni nani atakayelikomesha? Sasa, kama hiyo ni... Mnaona? Ni kitu gani? “Kila mmea ambao Baba Yangu wa Mbinguni hajaupanda utang’olewa.” Hivi ninyi...? Hivi hamwezi kuliadini Neno Lake kwa ajili yake? Lakini inatubidi kuunda yapata madhehebu thelathini na tano mbalimbali kuninii... .

“Vema, Yeye anakuja juu ya wingu jeupe.”

“La, Mungu abarikiwe, Yeye anakuja juu ya farasi mweupe.”

<sup>221</sup> Inaleta tofauti gani kwa vyovyote vile, almuradi anakuja? Jambo ndilo hilo. Mnaona? Lakini tumefanya nini? Tumekaa katika utaratibu ule ule wa kale: “Pokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha; pokea Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha; pokea Roho Mtakatifu,” mlima ule ule wa kale kwa miaka arobaini, utaratibu ule ule wa kale.

222 Lakini ni wakati wa kuinuka, hebu twende kaskazini. Yesu yuaa, hebu twende tukachukue kila ahadi. Haleluya! Kila ahadi! Yesu alisema, “Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya.” Yeye alinena kwa lugha, hiyo ni kweli, alifanya mambo mengine pia. Hebu twende tukaichukue ahadi.

223 Lakini, mnaona, Shetani ameona kanisa likienda bila Yesu, na kwa hiyo, hivyo ndivyo alivyowaona wakifanya, kwa hiyo akavuta pumzi yake ya sumu na kuanza “*Whiu!*” Akasema, “Sasa, nitawamaliza. Nimewaingiza katika hiyo miradi ya ujenzi na kadhalika, nami nitawazamisha moja kwa moja mle chini. Watakuwa wa kawaida, kila mmoja atakuwa na televisheni nyumbani mwake, na, ndugu, atakaa nyumbani Jumatano usiku. Kama hataenda kuona sinema, watu wa kale walikuwa wakisema, ‘Usiende kuona sinema,’ lakini nitaileta mumo humo nyumbani mwao. Mnaona?” Kwa hiyo anakuja tu moja kwa moja, mwajua, na kuyaleta mambo haya.

224 “Na kama wa—wakisema haiwavutii, lakini wanaangalia vipindi hivi, *Tunampenda Susi*, na mambo haya yote, watakipenda hicho zaidi, na mambo ya ulimwengu, kuliko wanavyompenda Mungu, najua watakipenda. Nami nitalivunjilia mbali kanisa lote la Kipentekoste.” Kulitikisa, kulisukuma, kulivunjavunja, makasia yamevunjika na kila kitu, hiyo ni kweli, hivyo ndivyo amefanya. Akawaona wakienda kombo kwenye miradi mikubwa ya ujenzi, wakizidi kuwa wa kilimwengu tu kama makanisa mengine. Hiyo ni kweli.

225 Kama nilivyosema, walizoea kusema, “Mbaptisti baridi, wa kawaida,” sasa ni, “Mpentekoste baridi, wa kawaida.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

226 Sisi hapa, tumerushwarushwa, lakini jambo zuri (sina budi kuharakisha, kufunga tu, maana wakati umewadia.), angalieni, jambo zuri lilikuwa kwamba Yeye hakuwa ameenda mbali sana. Alipanda juu ya mlima mrefu kuliko yote aliyoweza kupata, Naye alikuwa akiwaangalia huko nje baharini.

227 “Jicho Lake liko kwenye shorewanda, nami ninajua Yeye anaangalia.” Naam. Ni nini kilitukia? Alipanda Kalvari, akaendelea kupanda, tangu Pasaka, Yeye alipanda juu kuliko mwezi, nyota, moja kwa moja akaingia Utukufuni, kadiri unavyozidi kupanda juu ndivyo unavyoweza kuona mbali, kusudi aweze kuliangalia Kanisa la ulimwenguni kote, kila mahali. Akituangalia, macho Yake yako juu yetu.

228 Halafu yapata wakati ambapo matumaini yote yalikuwa yamekwisha ya kuwa na uamsho mwingine (Waliwazia nini wakati matumaini yote yalipokwisha?), Huyu hapa anakuja akiwaendea akitembea juu ya bahari. Loo, jamani! Akitembea juu ya bahari. Nao walipomwona Yeye, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, walikiogopa, walidhani kilionekana kama mzuka.

229 Na ndivyo ilivyo siku hizi, kitu pekee kinachoweza kulileta Kanisa pamoja, lipate Unyakuo, wanasema, “Ni kupiga ramli, ni Beelzebuli,” wakati jambo lile lile alilosema Yeye angefanya. Kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo sasa.

230 Lakini alisema nini basi? Laiti ningalikuwa na muda mrefu zaidi, lakini sina. Lakini Yeye alisema nini basi? “Msiogope; jipeni moyo; ni Mimi.”

“Unajuaje ni Yeye?”

Maana Yeye hutenda kama alivyotenda alipokuwa hapa, Yeye hufanya mambo aliyofanya, Yeye hutimiza ahadi Yake kama alivyoitimiza. Hiyo si ni kweli?

231 “Msiogope; ni Mimi; msiogope. Msiogope sasa; ni Mimi; jipeni moyo. Uwe na moyo wa ushujaa, jijenge, nimekukazia macho, ninaangalia. Ninakuja katikati ya Assemblies, katikati ya Church of God, ninaingia humu, nifanye nini? Kuwachukua Wateule, sio kufanya dhehebu lingine, bali Kunyakuliwa wapate kwenda Nyumbani; ninakuja kwa ajili ya hiyo.”

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

232 Mwokozi mbarikiwa, Wewe utatuongoza hata tutakapoifikia ile Pwani yenye afya, ambapo Malaika wanangojea kuungana nasi, katika sifa Zako milele. Tunawazia juu ya siku hiyo kuu, jinsi Wewe umeipanga.

*Ndugu, sitaki... msijue habari za hao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na hao wengine wasio na matumaini.*

*Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Kristo alikufa akafufuka tena siku ya tatu, vivyo hivyo na wale waliolala mauti katika Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye.*

*Kwa kuwa twawaambieni haya kwa amri ya Bwana, kwamba hatutatanguliwa, haitatuzuia wakati tumelala mauti.*

233 Tunaangalia utaratibu wa ufufuo: Jambo la kwanza, tunakusanyika, tukiisha kukusanyika ndipo tutaenda pamoja kumlaki. Mama na baba watakutana, watoto na wapendwa watakutana, kisha wanyakuliwe hewani kumlaki Bwana. Ndipo tutakaposimama pale, tukiimba nyimbo za ukombozi, nao Malaika, wakifanya duara kuizunguka dunia, watasimama huku wameinamisha vichwa, bila kujua wanachozungumzia. Hawakupotea kamwe, hawajui maana ya kupotea na kupatikana, lakini, Bwana, tunajua maana yake. “Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa nimepatikana, nilikuwa kipofu lakini sasa ninaona.”

234 Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utawabariki watu hapa Jumamosi hii usiku. Ujumbe mdogo, uliokatwakatwa kutoka tu

mahali hadi mahali, tukijaribu kungojea kuona kile ungesema kifanywe, sasa saa inakaribia.

<sup>235</sup> Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawafanya tu watu wajue ya kwamba Wewe ni Yesu yeye yule. Njoo tu na ufanye, usiku wa leo, kama tu ulivyofanya kule, kwa muda kidogo tu kwa ajili yetu, Baba. Kusudi watu . . . huenda kamwe wasipate nafasi nyingine. Huenda tusiwe na kanisa asubuhi, huenda Wewe ukaja kabla ya asubuhi, wakati fulani usiku, huenda kukatokea sauti, “Tazama Bwana Arusi yuaja, tokeni mwende kumlaki.”

<sup>236</sup> Tunajua utakuwa wakati wa kutisha sana wakati huo, kutakuwa na kulia, kutakuwa na kuomba, kutakuwa na kuimba, kutakuwa na kupiga makelele. Baba Mungu, jalia tujiweke sawa sasa, na tuwe tayari kwa ajili ya saa hiyo, tunapongoea, katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>237</sup> Sijui kama kuna yeyote hapa, usiku wa leo, asiyemjua Yeye kama Mwokozi, angetaka kusema, “Nikumbuke, Ndugu Branham, unapoomba tena.” Inua mkono wako, useme, “Nikumbuke.” Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, wewe. Katika roshani, Bwana awabariki. Mtu mwingine, kabla tu hatujawaombea wale wanaotaka kumjua Yeye, hujawahi kukutana Naye?

<sup>238</sup> Jalia . . . Huenda akaja katika dakika chache hapa. Atakuja, ninaamini atakuja. Nanyi je? Naye atafanya ninii Yake . . . Mnaamini Yeye ni yule yule? Hakika, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Basi jalia aje na kufanya, kupitia kwetu, kupitia kwa nguvu Zake za kutakasa, mambo aliyofanya alipokuwa hapa duniani, nasi tutajua. “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye. . . ”

<sup>239</sup> Hivi ninyi, ni wangapi wanaajua ya kwamba Yesu Kristo kamwe hakufanya mwujiza mmoja maishani Mwake, bila Mungu kumwonyesha kwa ono? Ni wangapi wanaojua hilo? Biblia inasema hivyo, Yohana Mtakatifu 5:19, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda.” Hiyo ni kweli? Sasa, hilo ni la Kimaandiko, haliwezi kuvunjwa. “Sifanyi neno mpaka nimwone Baba analitenda. Yoyote atendayo Baba, nami ninayatenda hata sasa. Yale Baba afanyayo, Yeye hunionyesha Mimi, halafu ninayafanya.” Yeye huigiza tu katika mchezo wa kuigiza yale Baba aliyomwonyesha kufanya, hiyo inamfanya Yeye yule leo, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.”

<sup>240</sup> Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi wakati huo, Roho yuyo huyo aliyekuwa ndani ya Masihi atakuwa katika Kanisa Lake, Kanisa litafanya mambo yale yale aliyofanya Masihi, maana mzabibu unaweza tu kuzaa zabibu kila unapochipuka, hivyo ndivyo ilivyo kwetu hapa, haina budi kuwa vivyo hivyo.

<sup>241</sup> Je, yule mvulana alisambaza kadi zozote za maombi? Hata nilisahau kuuliza . . . Naam. Jana usiku hakufanya hivyo. [Ndugu

fulani anasema, “Alisambaza chache, usiku wa leo.”—Mh.] Alisambaza chache, usiku wa leo. Unajua zilikuwa namba gani, herufi, ama...? [“A.”] A, nini? Hiyo ndiyo uliyosambaza? Sisi ni...? Hizo ndizo tulizokuwa nazo usiku wa kwanza, sivyo? Ulifanya nini, uligawa tu hizo hamsini zingine? Vema. Tulianzia wapi wakati huo mwingine? [“Moja hadi kumi na tano.”] Moja hadi kumi na tano. Vema, hebu na tuanzie mahali pengine miongoni mwao, usiku wa leo. Hebu tuanze...Walisambaza kumi na tano? [“Naam.”] Hebu na tuchukue hizo kumi na tano za mwisho basi, hiyo ingekuwa, mwanzo ungekuwa, huo ungekuwa ni nini? Themanini na tano, sivyo? Themanini na tano. Hebu tuone kama wao ni...sisi—sisi...kama wako huku.

<sup>242</sup> Themanini na tano. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba themanini na tano? Inua mkono wako, kote kote jengoni, mtu fulani, ama ghorofani, popote ulipo. Kadi ya maombi A, themanini na tano. Angalia ninii yako...[“Moja kwa moja mbele zako.”] Je, niliikosa? Mna hakika? [“Papo hapo mbele yako, hapo.”] Loo, samahani, dada. Vema themanini na tano, njoo hapa, papa hapa. Themanini na sita. Ni nani aliye na themanini na sita? Inua mkono wako. Kadi ya maombi themanini na sita.

<sup>243</sup> Tunaleta hizo kadi hapa chini mbele ya watu, tunazichanganya zote namna *hii*, kisha tunampa mtu yeyote kadi ya maombi anayetaka moja, kwa hiyo basi tunaposhuka, tunaita tu kutoka mahali fulani, bila kujua palikuwa ni wapi. Kwa hiyo, basi inaninii tu...

Ni wangapi wanaojua kuna wengi zaidi wanaoponywa katika kusanyiko, kuliko wanaoponywa hapa juu? Hakika, kunao. Bila shaka.

<sup>244</sup> Vema, vipi...? Zunguka upande *huo*. Vipi...? Hiyo ilikuwa wapi? Themanini na tano, sivyo? Themanini na sita. Ni nani aliye na kadi ya maombi themanini na sita, waweza kuinua mkono wako? Mama mmoja papa hapa. Una themanini na sita? Je, ungeambatana na huyo mama kule?

<sup>245</sup> Themanini na saba, inua mkono wako upesi sana sasa kuhifadhi...Mungu akubariki, ndugu yangu, zunguka moja kwa moja *hivyo*. Themanini na tano, themanini na sita, themanini na saba, themanini na nane. Ni nani aliye na themanini na nane? Papa hapa, zunguka upande *ule*. Hapo wamechanganyikana kote jengoni, mtu yeyote aliyetaka moja. Themanini na nane, themanini na tisa. Ni nani aliye na themanini na tisa? Kadi ya maombi themanini na tisa, inua mkono wako. [Mtu fulani anasema, “Moja kwa moja huko nyuma.”—Mh.] Huko upande wa...Wapi? [“Sawa.”] Kulia, themanini na tisa. Kamwe...Siwaoni, bali hebu wasimame na kuzunguka moja kwa moja upande huo, wakiweza, themanini na tisa.

246 Tisini. Ni nani aliye na kadi ya maombi tisini, waweza kuinua mkono wako? Angalia kadi ya jirani yako, huenda. . . mtu fulani kiziwi, mwajua, wasingeweza kuisikia, labda mtu fulani ni kiwete na wasingeweza kuinua mkono wao. Angalieni tu kila mahali kadi ya kila mtu.

247 Ati nini? Kadi ya maombi, hiyo ilikuwa ni gani, themanini na tisa? Tisini. Je, hiyo kadi ya maombi ni tisini? Vema, bwana, zunguka upande *huo*. Tisini, tisini na moja, sawa. Tisini na mbili, tisini na tatu. Inua mkono wako, ili nione wewe ni nani. Tisini na tatu. Waweza kuinua mkono wako? Tisini na tatu. Vema, tisini na nne, inueni ninii yenu. . . Hiyo ni kweli. Tisini na tano, tisini na sita, tisini na saba. Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Tisini na saba, tisini na nane, tisini na tisa, mia moja. Vema, sawa.

248 Sasa, kuna kadi zingine za maombi hapa ndani? Inueni mikono yenu, ninyi mlio na kadi za maombi. Vema, shikilieni tu kadi zenu, tutawafikia, tuliahidi hilo, tutawafikia. Mnaona? Kwa msaada wa Bwana, tutazifikia.

249 Hii ni ninii tu. . . Hatuwezi kuwaleta wote mara moja. Mimi, kesho alasiri itanibidi kuzichukua zote, mnaona, kwa hiyo nitakuwa na alasiri ya kufanya hivyo, mnaona. Kwa hiyo, njoni tu, nasi tuta—tutawafikia.

250 Na sasa, ni wangapi wasio na kadi ya maombi? Inueni mikono yenu. Nanyi ni wagonjwa na mnataka Mungu awaponye? Inua mkono wako, useme, “Sina kadi ya maombi, bali hata hivyo nataka Bwana aniponye.” Vema, ni kila mahali tu kwa jumla.

251 Vema. Wakati wakitayarisha mstari wa maombi, nitamwomba kila mtu, kama mtakuwa na kicho tu mwezavyo, na kukaa vitini mwenu, endeleeni tu kuketi, mnaona. Vema.

252 Sasa, katika Biblia, katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu mlango wa 4, ningetaka kusema hivi: Ni wangapi waliowahi kusoma mlango wa 4 wa Yohana Mtakatifu? Vema. Sasa, Yesu, la, samahani, si mlango wa 4 wa Yohana Mtakatifu, siwezi kuukumbuka sasa hivi. Wakati yule mwanamke alipoguswa akiwa na kutokwa kwake kwa damu, nimeusahau tu akilini mwangu, mlango wa 8.

253 Kwa hiyo alikuwa akipitia kwenye umati wa watu, naye akasema. . . alikuwa amemwona na kusikia habari za Yesu, kamwe hakuwa amemwona. Lakini hebu tuchukue tu mchezo mdogo wa kuigiza wakati wakingojea pale. Ninaweza kuwazia, alikuwa—alikuwa akitokwa na damu, kila mtu anajua kilichokuwa kimetukia, ilikuwa ni wakati wa kukoma hedhi, wala haikukoma. Kwa hiyo yeye, naye alikuwa ametumia pesa zake zote kwa madaktari, wala wasingeweza kumsaidia hata kidogo. Walikuwa wamefanya yote waliyoweza kufanya, hapana shaka, walikuwa wamefanya kila kitu walichoweza kufanya, bali wasingeweza kukomesha kutokwa huko kwa damu.

<sup>254</sup> Basi alikuwa na hiyo kwa miaka mingi, mingi sana, na ikaendelea tu, ikifurika, zaidi, zaidi, zaidi, maskini, mtu duni, dhaifu, alikuwa amesikia habari za Yesu, kwa hiyo akasema, “Ninaamini Yeye ni. . . Yeye ndiye yule Masihi.” Hivi hudhani yeye aliwazia hilo? Ni wangapi wanaoamini hilo? Semeneni, “Amina.” [Makusanyiko yanasema, “Amina.”—Mh.] Akasema, “Ninaamini Mtu huyo ndiye Masihi, bali sina pesa za kwenda mahali Yeye alipo.”

<sup>255</sup> Lakini mnajua, baada ya tukio hili kuu la huo usiku, Yeye alikuwa amekuja kwenye, hiyo mimea ya majini kule chini asubuhi hiyo. Ndipo akaangalia chini ya kilima alimoishi, akasema, “Nashangaa Huyu ni Nani. Kitu fulani, hapana shaka kuna Mtu fulani kule chini.” Akawasikia wakipiga makasia, na kumdhihaki, na kadhalika, na wengine wakimbariki, na kwa hiyo akatelemka kisiri na kuona Huyu alikuwa ni nani. Naye akasema, “Kama ninaweza tu kugusa vazi Lake, nitakuwa mzima.”

<sup>256</sup> Sasa, yeye hakuwa na hata sehemu moja ya Maandiko kwa jambo hilo, siyoy? Kuna Andiko lolote katika Biblia kabla ya hapo, linalosema, “Ajapo Masihi, kama mtaligusa vazi Lake. . .” La, bali aliamini, aliamini, kwa hiyo akajipenyeza kupitia kwenye huo umati, naye alikuwa ni maskini mwanamke mkongwe, mwembamba sana, mwajua, kwa hiyo akajipenyeza tu katikati ya huo umati, ndipo akagusa vazi Lake.

<sup>257</sup> Sasa, kama uligusa koti langu, nisingelihisi, koti langu tu. Nalo vazi la Kipalestina lilikuwa ni joho. Nao walikuwa na vazi la ndani, lililotoka mguuni kwenda juu, hiyo ndiyo sababu walikuwa na kutawadha miguu, na kadhalika, joho hilo kubwa lilikota mavumbi walipokuwa wakitembea kwenye vijia.

<sup>258</sup> Vema, basi, kama uliwahi kuwa Palestina, na kuona jinsi walivyofanya, jinsi wanavyovua viatu vyao, na kuoshwa miguu yao kwa sababu ya uvundo wa ardhi walimokuwa wanyama, na kadhalika, hawakupendeza kwa watu, kwa hiyo walikuwa na—walikuwa na mtumishi aliyetawadha miguu, na kwa hiyo walikuwa na kutawadha miguu.

<sup>259</sup> Kwa hiyo mwanamke huyu aligusa upindo wa vazi Lake, likining’inia mbali *hivyo* kutoka Kwake. Sasa, kimwili, asingeweza kuuhihi, asingeweza kuuhihi. Lakini aliugusa upindo wa vazi Lake, kisha akaondoka, akaketi chini, akasimama, ama chochote kile katika kusanyiko la watu, labda mara mbili au tatu ya walio hapa.

Yesu akasimama, akasema, “Ni nani aliyenigusa?”

<sup>260</sup> Mbona, Petro alidhani hiyo ilikuwa ni dhahaka, hakuwa amempokea Roho Mtakatifu bado, mwajua, mtu aliye na Roho Mtakatifu angejua vinginevyo. Kwa hiyo, akasema, “Kwa nini. . .?” Mbona, Biblia ilisema alimkemea. Kwa maneno mengine, alisema, “Unamaanisha nini kusema jambo kama

hilo? Unadhaniwa kuwa Mtu mwenye busara, na hapa Wewe uko hapa, unajiita Mwenyewe Masihi, na kusema, ‘Ni nani aliyenigusa?’ Mbona, hivi hujui watu watafikiri Wewe una kichaa? Kila mtu anakugusa Wewe.”

Ninaweza kumwona Yesu akimwanguka, kawazia, “Maskini Simoni.”

<sup>261</sup> “Lakini huu ulikuwa mguso wa namna nyingine, Simoni, naona kwamba nimekuwa dhaifu.” Nguvu, uweza ulikuwa umemtoka, Naye akasimama tu. Aliona Simoni hakujuu, na hao wengine hawakujua, kwa hiyo alianguka tu huku na huku juu ya kusanyiko mpaka akamwona mwanamke huyo, labda ameketi huko nyuma kabisa. Akamwambia kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma, kwa sababu imani yake ilikuwa imemwoko. Hiyo ni kweli?

<sup>262</sup> Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba Agano Jipya lilisema ya kwamba Yesu Kristo, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu, ameketi mkono wa kuume wa Mungu, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Basi je, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? Basi ungejua je ulingusa? Yeye angetendaje? Angetenda kama tu alivyotenda wakati huo, kama ni Yeye yule.

<sup>263</sup> Kwa hiyo ninyi msio na kadi zenu, ama chochote kile huko nje kwenye kusanyiko ambao hamtakuwa hapa usiku wa leo, ombeni tu, na kusema, “Bwana Yesu, ninaamini Wewe ndiwe yule Kuhani Mkuu ambaye wanazungumza habari zake, basi jalia imani yangu ikuguse Wewe, usiku wa leo.”

<sup>264</sup> Sasa, kama ulinigusa, isingefaa kitu zaidi ya kumgusa mumeo, ama kumgusa ndugu yako, ama—ama—ama mwanao, ama chochote kile, unaona. Hilo halingefaa kitu, kunigusa mimi, haingekuwa kitu. Lakini wewe mguse tu Yeye, kisha uangalie yale afanyayo.

<sup>265</sup> Unasema, “Ndugu Branham, angetendaje?” Kwa karama, kujitolea tu kwa Roho, Yeye huzungumza. Mnaona? Sasa, maikrofoni hii ni bubu kabisa, haiwezi kunena, haijui kuzungumza, inahitaji kitu fulani kuizungumzia, kuifanya ibebe sauti. Hiyo ni kweli?

<sup>266</sup> Vema basi, hatufahamiani na yeyote wenu hapa. Watu wawili tu ninaowafahamu hapa ni hawa, mtu huyu aliyeketi hapa alikuwa pamoja nami asubuhi ya leo, na Ndugu Gene Goad, na mtu huyu hapa, na Ndugu Hall, aisee, hao ndio tu ninaoweza kuwaona humu jengoni; mke wangu hayupo hapa, usiku wa leo. Na hao ndio tu niwajua. Lakini Yesu anajua kila mmoja wenu. Hiyo ni kweli? Yeye anajua kila mmoja wenu. Naye aliahidi, katika siku za mwisho kutakuwako Nuru, kama tu ilivyokuwa wakati wa kuchomoza kwa jua, itakuwa vivyo hivyo

katika kutua. Hiyo ni kweli? Sasa, wewe gusa tu vazi Lake, kama atakuja na kutusaidia.

<sup>267</sup> Basi wangapi wenu walio wageni hapa, ambao hawajawahi kuliona hapo kabla, wangemwamini Yeye, na kusema, “Ingenifanya niamini kumwona Yeye akitenda kama vile tu alivyotenda alipokuwa hapa duniani”? Inua mkono wako, useme “Ni—nitaamini.” Hao ni wageni ambao hawakuwa hapa hapo awali. Vema. Hilo ni sawa.

Ni wangapi wamekuwa hapa hapo awali na kumwona akifanya hivyo? Hebu tuone mkono wako. Mnaona? Ni karibu kila mahali. Vema. Sasa, wewe amini.

<sup>268</sup> Sasa, kumbukeni, kama mtu mmoja akija, Naye amponye mtu huyo, Yeye—Yeye hana budi kufanya hivyo kwa mtu wa pili anayekuja kwa msingi ule ule. Kweli. Kama utaamini tu, inahitaji imani yako. Wasema, “Vipi kuhusu kundi lile lote pale siku ile? Mwanamke mmoja tu ndiye aliyemgusa.” Huyo ndiye pekee ambaye angeweza kuamini hilo. Je, wewe ni huyo mmoja huko nje, usiku wa leo? Natumaini ndivyo mliyvyo, kila mmoja wenu. Sasa, kumbukeni tu . . .

<sup>269</sup> Sasa, Baba Mungu, nimenena habari Zako, nimejaribu kuliweka katika mfano mdogo wa hadithi, usiku wa leo, katika mchezo wa kuigiza, ili kwamba hata watoto wadogo wapate kuelewa, hata wangeweza kuwaambia maskini wanafunzi wenzao, na kadhalika, na wote wangeweza kuwa tayari kwa ajili ya kuja kwa Bwana.

<sup>270</sup> Sasa, nimenena, nimekushuhudia Wewe, hayo tu ndiyo niwezayo kufanya, mimi ni mwanadamu tu. Lakini sasa, Baba, Neno moja tu kutoka Kwako litamaanisha yote, zaidi ya vile sisi sote tungeweza kufanya katika nyakati nyingi za maisha, Neno moja tu. Wanajua ni Maandiko, wanajua ni kweli, wanajua ni kutoka Mwanzo hadi Ufunuo.

<sup>271</sup> Sasa, Wewe ulitoa ahadi ya kwamba Masihi ajaye, katika siku hizi, angerudi Kanisani, na kufanya tu kama alivyofanya, ninii . . . wakati alipoweka . . . Kuja tu kwa lile Jiwe la kuwekwa juu, lile Jengo lingetengenezwa kwa ajili Yake.

<sup>272</sup> Ninaomba, Mungu, ya kwamba itakuwa hivyo tena, usiku wa leo. Kwa kuwa tunaomba, hayo katika Jina la Yesu, ninapojisalimisha Kwako, na kuchukua kusanyiko hili na kila roho humu ndani, chini ya udhhibiti wa Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

<sup>273</sup> Vema. Sasa, aminini. Kila mtu awe na kicho, aketi kwa utulivu. Usikose kuamini, bali amini kwa moyo wako wote.

<sup>274</sup> Sasa, sasa ni shindano la kuamua, nililithubiri. Ni wangapi wanajua ilikuwa ni Neno? Sasa, kama yeyote wenu anashuku, mbona umekaribishwa kuja hapa na kuchukua mahali pang ukitaka. Mhudumu fulani hapa aseme, “Si sawa, si sahihi,” basi

wewe njoo hapa na uchukue mahali pangu na kufanya jambo lile lile.

<sup>275</sup> Kama ninawatoa pepo kwa Neno la Mungu, ninyi mnawatoa kwa nani? Unaona? Kama unaweza kufanya vizuri zaidi, mbona, njoo, nitaketi chini; ninataka kuona watu wakiponywa. Mmelipata? Mnaona? Ni ahadi ya Mungu. Na kama atatimiza ahadi hii. . .

<sup>276</sup> Sasa, tunajua, hebu niweke jambo hili dhahiri, hakuna mtu anayeweza kumponya mwingine, hata hakuna dawa inayokuponya. Hakuna daktari atakayekwambia hivyo kama yeye ni daktari halisi. Dawa haijengi tishu, dawa husafisha huku Mungu anajenga tishu, hana budi kuumba, tishu huumbwa. Mnaona? Kwa hiyo hafanyi hivyo, daktari haponyi mfupa, *anaurudisha* huo mfupa, Mungu anaiponya hiyo mifupa. Mnaona? Mungu pekee ndiye anayeweza kuponya. Na sasa, Yeye tayari amefanya hilo. Ili tu kuwafanya watu waamini hilo, hilo ndilo.

<sup>277</sup> Kama ingekuwa ni mimi, kama nilikwambia, hukuamini, ama kama uliniambia wala sikuamini, mwache aende. Lakini si Mungu, Yeye ni Mungu mwema. Yeye anaendelea kutuma karama, na kuziweka Kanisani Mwake kulingana na Neno Lake ili kulithibitisha Neno Lake na kulifanya kweli, ili kwamba awe mwenye haki na mwaminifu.

<sup>278</sup> Sasa, mama huyu anayesimama hapa, ama, nadhani wewe ndiye, wa ku—kuombewa. Sasa, huyu hapa mwanamke amesimama ambaye sijawahi kumwona maishani mwangu nijuavyo mimi. Hatufahamiani, nadhani. [Huyo dada anasema, “Nimekuona Ndugu Branham.”—Mh.] Uliniona. [“Uliniombea katika kanisa lako dogo.”] Nilikuomba? [“Tennessee. Naam, uliniomba.”] Huko Tennessee. [“Naam.”] Vema, nina furaha sana kwa jambo hilo. Lakini kukujua, nisingekujua, nisingekuwa na njia ya kukujua. Vema.

<sup>279</sup> Sasa, mama huyu anasema, kama hukunisikia. . . Na jambo lingine, yeyote yule mhandisi wa hii, upako ujapo, na endapo sizungumzi kwa sauti kubwa vya kutosha, iongeze ili waweze kuisikia. Maana, unaona, kurudi tu katika maisha ya mtu fulani kwa miaka, na kuona yale ambayo wamefanya, nawe unaangalia tu kinachoendelea pale, ha—hata hutambui kwamba umesimama hapa.

<sup>280</sup> Sio mimi. Ningewezaje kufanya hivyo? Haiwezekani kabisa. Ni—ni mwujiza mkamilifu kama ingetendeka. Limepita hoja zozote za kibinadamu, isipokuwa uamini Neno la Mungu kwake. Bila shaka. Ndio mwujiza ulio mkuu kuliko yote.

<sup>281</sup> Unasema, “Vema, huyu hapa mtu fulani ameketi hapa aliyekuwa na mguu uliolemaa, tulimwomba, akaanza kutembea.” Vema, hiyo inaweza kuwa ni saikolojia, hiyo ni

kweli. Lakini hii haiwezi kuwa, haina budi kuwa ni Mungu, hakuna kitu kingine kinachoweza kuwa hivyo. Kweli kabisa.

<sup>282</sup> Kwa hiyo sasa, kama nilikuombea, na kwamba... Lakini sikujui, wala sijui lolote kukuhusu, sina fununu ya kilichokuleta hapa. Nawe, kama tu vile, kama mtu fulani niliyemwomba hapa angenijia katika miaka kadhaa tangu sasa, na kusema, “Nilikuwa huko Richmond, Virginia, nawe ukaniombea.” Loo, jamani, nimewaombea makumi elfu, mara maelfu ya watu, mnaona. Na, kwa vyovyote vile, kama ungekuja kwangu kesho, kisha upako uje na ono lije, ukija kwangu kesho, nisingejua lolote kulihusu.

<sup>283</sup> Mnamwona yule mvulana aliyeketi pale? Yeye anarekodi, hivyo ndivyo tunavyoweka kumbukumbu zake. Hiyo si ni kweli, Ndugu Goad? Hivyo ndivyo tu nijuavyo. Mnaona? Kwa sababu si mimi ninayezungumza. Ni—nimekiri na kuinua mikono yangu kwamba simjui. Unaona?

<sup>284</sup> Lakini kama ulikuwa mgonjwa nami nikaweka mikono yangu juu yako, na kusema, “Biblia ilisema wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya,” hivyo ndivyo tumekuwa tukifanya kwa miaka mingi, bali tumekaribia Nyumbani zaidi sasa, mnaona, Kristo anadhihirishwa zaidi kwetu.

<sup>285</sup> Sasa, kama Yeye ataniambia jambo fulani ambalo—ambalo limekuwa maishani mwako, vema, basi, kama akikwambia kile kilichokuwako, utakuwa hakimu kujua kama hiyo ni kweli ama si kweli, utajua, unaweza kuliambia kusanyiko hili, ni kweli ama si kweli. Vema, basi, kama Yeye akifanya hivyo, na anajua kile kilichokuwako, hakika Yeye angejua kile kingekuwa. Je, hiyo ni kweli, enyi wasikilizaji? Angejua kile kingetukia. Sasa, sasa, sijui kwamba atafanya hivyo, bali ninatumaini ya kwamba atafanya hivyo, na kama atafanya, Mungu asifiwe.

<sup>286</sup> Ndipo, kila mmoja wa kusanyiko, tunaposimama hapa, wazi, taa kubwa zikituangazia, tunasimama hapa, bila chochote ila Neno la Mungu limewekwa hapa mbele zetu, Mungu Mwenyewe, tuko katika Uwepo Wake mbele ya watu mia tano ama mia sita au zaidi, nadhani, na, wowote wanaotoshea hapa mahali padogo, na sisi hapa. Ilifanya hivyo mbele ya laki tano wakati mmoja, laki tatu wakati mwingine, na mamia ya maelfu mara nyingine, mataifa ya kila namna, na jamaa, na lugha. Mnaona? Hili halina budi kwenda kila mahali; Yeye hana budi kujitangaza Mwenyewe kabla hajaja.

<sup>287</sup> Sasa, hii ni kama tu ilivyokuwa katika wakati wa Biblia wakati Bwana wetu alipokutana na mwanamke Msamaria, nasi ni mwanamume na mwanamke wamekutana hapa, sikujui, nawe unanijua tu kwa kupitia mstarini wakati mmoja. Sasa, kama Yeye akinifunulia kilichokuleta hapa, huenda ni mgonjwa tena, huenda ikawa ni shida ya kinyumbani, huenda ikawa ni shida ya

kifedha, sijui, lakini Yeye anajua, lakini kama Yeye atanifunulia kile kilichokuleta hapa, utaamini, sivyo?

Nalo kusanyiko litaamini? Mtaamini? Hakika. Vema. Na atujalie.

<sup>288</sup> Sasa, kama watu wangali wanaweza kuisikia sauti yangu, huyu mwanamke ananiondokea. Naam, ninakuona, uliponywa. Uliponywa katika mkutano wangu, ulikuwa na yabisi kavu na ukaponywa, ndivyo hivyo, hiyo ni kweli. Uh-huh. Um-hum.

<sup>289</sup> Sasa, mguu una shida fulani. Ulianguka na kuumiza mguu wako, hiyo ndiyo—hiyo ndiyo uliyokuja hapa kuombewa. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Inua tu mkono wako, ili wapate kuona. Um-hum.

<sup>290</sup> Unaamini? Vema. Sijui ni kwa nini, lakini ninaendelea... Sasa, kile mnachowazia, ninakipata hapa. Mnaona? Hivi Yeye aliwaangalia watu na kutambua mawazo yao? Hiyo ni kweli. Vema, mnaona, huyo ni Yeye, sio mimi, tayari nimewaambia, mimi, si mimi tena, ni Yeye sasa. Huyu hakuwa ni mimi niliyemwambia hivyo, Huyu ni Yeye aliyemwambia hayo, maana simjui, Mungu anajua hilo. Sasa, wanaendelea kufikiria nilibahatisha; sijui ni kwa nini inakuja, lakini inatoka mahali fulani. Naam, ninaona mahali inakotoka sasa, ninapaswa kuwataja. Ninasema kweli? Angalieni kama ilikuwa hivyo.

<sup>291</sup> Naam, naam, naona ulianguka na kujiumiza, ukaumiza kiungo chako. Nawe umejaribu kila kitu kwa ajili yake, dawa za kuchua, na chochote kile, lakini haitafaulu, hii itafaulu.

<sup>292</sup> Umekuwa na huzuni nyingi, umempoteza mpendwa, huyo alikuwa ni binti. Hiyo ni kweli. Um-hum. Um-hum. Kama Mungu ataniambia wewe ni nani, jina lako ni nani, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, mtumishi Wake? Bibi Wathen, nenda ukaamini, Yesu Kristo anakuponya. Mungu akubariki sasa. Itakuwa sawa, maumivu yatatoweka, nawe utakuwa mzima.

<sup>293</sup> Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, ninamwuliza mtu yeyote, ningeweza je kamwe, tatizo lolote lililompata huyo mwanamke, alichowahi kufanya? Inabidi kuwe na namna fulani ya Kiumbe cha kimbinguni hapa kinachofanya hivyo (Mimi ni mwanadamu. Hiyo ni kweli?), Ni nani angemjua mwanamke huyo, yale aliyofanya, mahali amekuwa, na yote kumhusu, na mambo kama hayo.

<sup>294</sup> Sasa, kama tungenimama hapa, kadiri unavyosimama muda mrefu zaidi, ndivyo mengi yangesemwa. Lakini mnaona, hilo moja—ono hilo moja liliondoa nyingi kwangu kuliko ile saa moja na nusu ya mahubiri. Mnaona? Unaingiza, sasa unatoa nje.

<sup>295</sup> Wazia tu, kama mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, naye... Yeye alisema, “Naona kwamba nguvu zimenitoka,” ingenifanyia nini mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, ingenifanyaje? Mnaona? Kwa sababu Yesu alisema, “Kazi

nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya, na nyingi kuliko hizi mtazifanya.” Ninajua la King James linasema, *kubwa zaidi*, bali zisingeweza kuwa kubwa zaidi, zilikuwa ni *nyingi zaidi* za kazi ambazo Yeye angeweza kufanya. Chukua *Diaglott* asili, uone kama haisemi *nyingi zaidi*, unaona, kwa kuwa ni Roho yule yule.

<sup>296</sup> Sasa, hatufahamiani na mama huyu pia. Sikujui, lakini Mungu anakujua. Kama Mungu atanifunulia jambo ambalo ndilo shida yako, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Sasa, unajua ya kwamba jambo fulani ndio kwanza litukie wakati uo huo, unaona. Hiyo ilikuwa ni hisia hiyo na kama utamu, tulivu. Sasa, kama hiyo ni kweli, kusudi tu watu wajue, ili kwamba wajue ya kwamba sisemi jambo lolote baya, niliona hiyo Nuru ikishuka moja kwa moja juu yako, hiyo ni kweli, sasa, kama unahisi kitu kama hisia tamu sana, nyenyekevu karibu nawe, inua mkono wako ili watu wauone.

<sup>297</sup> Lakini kwenu mlilo na picha hapa, tunayo, Nuru ile mnayoiona kwenye picha, Mungu ndiye Hakimu wangu, iko moja kwa moja juu ya huyu mwanamke sasa. Mnaona? Naam, bwana.

<sup>298</sup> Yuko hapa, si kwa ajili yake mwenyewe, ingawa ana wasiwasi na fadhaa. Hiyo ni kweli. Shida ndogo ya akina mama imekusumbua kwa muda, lakini sababu kubwa iliyokuleta hapa ni mtu mwingine, huyo ni mumeo, amepooza kwa sehemu, ana shida mgongoni mwake na miguuni mwake. Hiyo ni kweli. Unaamini pamoja nami ya kwamba Mungu atampa afya? Nenda, na kama ulivyoamini, ndivyo itakavyokuwa kwako. Nenda ukaamini. Mungu akubariki. Iweke lesa hiyo uliyo nayo mikononi mwako juu yake. Amini tu kwa moyo wako wote.

<sup>299</sup> Mimi na wewe hatufahamiani, mama, nadhani. Hatufahamiani, lakini Mungu anatumia sote wawili. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake kwa moyo wako wote? Kama Mungu atanifunulia jambo ambalo ni shida, je, utakubali kwamba limetoka kwa Mungu? Ni mgongo wako, miguu yako. Imesababishwa na ajali. Vema. Hilo tu ndilo linalohitajika kukufanya mzima. Nenda, amini sasa, a—amini tu.

<sup>300</sup> Unaamini kwa moyo wako wote, mama? Unaamini ya kwamba Yesu Kristo atakutimizia haja yako? Bila shaka umevaa miwani, mtu yeyote angejua hilo. Hiyo imekuwa ni muda mrefu, tangu unapoweza kukumbuka, huo umekuwa maishani mwako mwote, lakini kwa kweli, hilo silo lililo moyoni mwako, kitu kingine moyoni mwako, hicho ni kwa ajili ya mtu mwingine. Hiyo ni kweli. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kumponya, ampe afya, mama yako? Ana ugonjwa wa kupooza, kutetemeka. Hiyo ni kweli, siyoy? Nenda, amini, itakuwa jinsi ulivyoamini. Mungu akubariki.

<sup>301</sup> Unaamini sasa kwa moyo wako wote? Je, inatosha kwako? Je, umeshawishika? Sasa, kuna nini hapa? Yule yule aliyetembea

Galilaya yupo hapa, usiku wa leo. Ni kitu gani? Yeye anatutumia tu mimi na wewe. Sasa, haijalishi ni—ni nini ingetiwa mafuta juu yangu, haina budi kuwa juu yao, pia, mnaona, haina budi kuwa juu yao, pia. Unaamini hilo? Amini tu. Usiwe tu na shaka, amini.

<sup>302</sup> U hali gani? Hatufahamiani, nadhani. Sikujui, lakini Mungu anakujua. Mtu mwingine alitokea katika lile ono, wakati uo huo tu, wakati lilipoanza kwa yule mwanamke. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Mambo ambayo nimesema ni kweli? Mungu atanifunulia shida yako ni nini, je, utanikubali kama mtumishi Wake? Vema. Una tatizo mgongoni mwako, hilo ni jambo moja, jambo lingine, umetiwa uvuli na mauti kwa kansa. Unaamini ya kwamba atakuponya, na kukupa afya? Unaamini.

<sup>303</sup> Mtu mwingine unayetaka aombewe, pia, sivyo? Unaamini Yeye atamponya, pia? Huyu ni mume wako, ameketi huko nje. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Je, utaniamini kama nabii Wake kama nikikwambia hilo? Ana shida ya matumbo, anasema daktari, ugonjwa wa matumbo. Kama unaamini ataponywa, pia.

<sup>304</sup> Lakini hili hapa jambo kuu sana unalohitaji: Unahitaji wokovu kwa ajili ya nafsi yako. Je, utamkubali kama Mwokozi wako, na kumwamini kwa moyo wako wote? Nyote wawili mnauhitaji. Utafanya hivyo na kuamini kwa moyo wako wote? Utamkubali kama Mwokozi wako sasa, kwa ajili ya uponyaji wako? Ewe mume, utamkubali kama Mwokozi wako? Mungu awabariki. Nyote wawili mmeokolewa na kuponywa pia. Nendemi nyumbani mkafanywe. . .

Mnaamini?

Unasema, “Huna haki ya kuwaambia wameokolewa?”

<sup>305</sup> Nadhani kama huyo Mungu anaweza kuniambia shida yao, Yeye anaweza kuniambia kama wameokolewa au la, sivyo? Bila shaka. Loo, mnampenda?

Je, unataka kwenda nyumbani, ule chakula chako cha jioni, upone ugonjwa huo wa tumbo, upate afya? Nenda ukale. Yesu Kristo anakuponya. Amini.

Njoo, bwana. Unataka Mungu akuponye ugonjwa huo wa mgongo? Endelea tu kutembea, ukisema, “Asante, Bwana Yesu,” na upate afya.

Yabisi kavu, wasiwasi, na kadhalika. Unaamini Yeye atakuponya? Sema, “Asante, Bwana.”

Ni wangapi wanaoamini kwa moyo wenu wote?

Amini, usiwe na shaka. Amini tu kwa moyo wako wote.

<sup>306</sup> Wanasema una mwuaji namba moja, lakini ugonjwa wa moyo si mwuaji namba moja, dhambi ndiyo mwuaji namba moja. Kwa hiyo, umeondolewa yote mawili sasa, kwa hiyo unaweza kwenda ukaponywe. Amini.

Tumbo lililokacha, ni sawa. Nenda, amini.

<sup>307</sup> Ninakuona ukijaribu kuamka asubuhi, ukitoa miguu yako uone kama unaweza kuamka vizuri, au la, maskini ibilisi huyo anayelemaza. Nenda, amini sasa, itakuacha, yabisi kavu itatoweka.

<sup>308</sup> Ingekubidi kufanyiwa upasuaji, mama, isingalikuwa ni Mungu. Unaamini Yeye anaweza kufanya upasuaji? Mwamini kabisa, uyasalimishe maisha yako yote Kwake, na huo uvimbe utatoweka? Unaamini hilo? Nenda, kama ulivyoamini, na iwe kwako. Nenda tu ukiamini. Vema.

Njoo, mama. Una ugonjwa wa wasiwasi, tumbo. Nenda, ukiamini, amini tu.

Njoo, mama. Unaamini kwa moyo wako wote? Hebu kidogo, jambo fulani lilitukia.

<sup>309</sup> Iweni tu na kicho, ngojeni tu kidogo, iweni na kicho. Loo, ni wakati wa jinsi gani! Je, Yeye . . . ? Ni mwanamke, aliyejitokeza, sio kama mwanamke huyu, yeye ni mwembamba zaidi, bali yuko kwenye kusanyiko. Mungu anisaidie. Naam, huyu hapa ameketi papa hapa. Una shida kwenye mikono yako. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, kwa tatizo la mkono? Vema, imani yako inakuokoa.

<sup>310</sup> Aisee, jambo lingine, weka mkono wako juu ya mwanamke huyo aliyeketi karibu nawe hapo, ana ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako, mpokee Kristo kama Mponyaji wako. Mungu awabariki. Nenda nyumbani, uwe mzima.

Yeye si ni wa ajabu?

<sup>311</sup> Hilo lilimfanya mama yule aliyeketi pale amevaa nguo hiyo ya samawati, akiugua ugonjwa wa tumbo, kuamini, pia. Umekuwa na ugonjwa wa tumbo kwa muda, sivyo? Nenda ukale chakula chako cha jioni, Yesu Kristo anakuponya.

<sup>312</sup> Huyu mama mnene, aliyeketi papo hapo karibu nawe, waweza kunipa fadhili, ama, kumpa Mungu fadhili? Wewe ni mwaminio, la sivyo Yeye asingesema nawe kamwe. Ana yabisi kavu, sivyo, mama? Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema, weka mkono wako juu yake, Dada. Nyote wekeaneni mikono hapo, Yesu Kristo anawaponya.

Mnaamini?

Unafikiri Mungu anaweza kuponya kisukari? Vema, endelea basi. Iweni na imani, Yeye atafanya hivyo.

Ugonjwa wa moyo? Endelea tu kusonga mbele, ukisema, "Asante, Bwana Yesu kwa kuniponya."

Una shida ya mgongo wako? Sema, "Asante, Bwana kwa kuniponya."

Loo, Yesu ni wa ajabu, sivyo?

313 Unawazia nini juu yake ukiketi hapo, maskini mama, unayeniangalia? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Basi hilo shinikizo la chini la damu litakuacha.

314 Mama aliyeketi moja kwa moja nyuma yako, uliwazia nini juu ya jambo hilo, bwana, wakati alipomwangalia? Huyu mama papo hapo nyuma yako, maskini mama huyo aliyevaa miwani, wewe pia ulikuwa na shinikizo la chini la damu. Hiyo ni kweli. Walipoweka kitu hicho mkononi mwako, alikwambia ulikuwa na shinikizo la chini la damu. Hiyo ni kweli? Kama ni kweli inua mkono wako. Nilijua je kwamba alifanya hivyo?

Amina. Unamwamini Yeye?

315 Kuvimba kwa mishipa, unaamini Mungu atakuponya? Vema. Una kadi ya maombi? Vema, si lazima uitumie. Umeponywa. Nenda, amini hilo.

316 Papo hapo nyuma, yabisi kavu, uliyeketi moja kwa moja hapo nyuma, wa pili aliyeketi. Unaamini Mungu atakuponya? Unaamini? Ukubali. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Asante, mama, kwa kusema hivyo. Nenda, ukaponywe.

317 Ee Mungu! Anaweza kufanya nini zaidi? Ni nini zaidi anachoweza...? Tayari amekuponya, alijeruhiwa kwa makosa yenu, akachubuliwa kwa maovu yenu. Sasa, mnatambua ya kwamba hilo jambo lote ni, inaonekana tu kama Nuru kubwa kote jengoni sasa. Mnaona, si—siwezi kuona kitu huko nje, ni vigumu. Ni ninii tu... Utukufu! Kama ningeweza... Laiti mngaliweza kutambua tu ya kwamba huyo ni Yeye! Hali fulani...

318 Mnasema, “Ndugu Branham, ni kitu gani kinachokufanya...?” Siwezi kuwaambia. Lakini hayo yalikuwa ni maono ishirini ama ishirini na matano yaliyotukia hapa jukwaani, wakati moja lilimfanya dhaifu, lingenifanyia nini mimi? Mnaiona neema Yake? Anataka ninyi nyote mliamini.

319 Unaamini hilo? Unaliamini kwa moyo wako wote? Je, utakubali kwa moyo wako wote? Basi simama kwa miguu yako, na umkubali Yeye kama Mwokozi wako, kama Mponyaji wako, kama Mbatizaji wako. Nami ninawakabidhi kwa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, Mungu wa Mbinguni na amwage Roho Wake juu yenu. Inueni mikono yenu mkampe sifa, na sasa mmeponywa.



61-0311 Msiogope  
Lyric Building  
Richmond, Virginia Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)